Pambazuko

Toleo Namba 085

Jumatatu, Agosti 19 - 25, 2024

Fuatilia mfululizo wa makala za Afcon kila Jumatatu Uk. 33

Gazeti Maalum la Afcon 2027

Lissu aweka masharti kujiunga CCM



● Mchungaji Msigwa atumika kwenye kandarasi ya kumng'oa Chadema

Habari Uk. 6 & 7

Naibu Rais wa Kenya mwiba Serikali ya Ruto

HISTORIA ni kama inajirudia kwani kile kilichomkuta William Ruto wa Kenya wakati...

Soma zaidi Uk. 21



Othman: Katiba ya Jamhuri mtego kwa Muungano

Uk. 16

Soma Ndani

Maono, falsafa za Rais Samia sasa kitanzini

MAONO na falsafa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya 4R, vimeingia majaribuni kufuatia kuwepo kwa matukio ya kukiukwa kwa haki za binadamu, utu na ustarabu wa Watanzania.

4R

Habari Uk. 8

Wamasai 'wakinukisha' Ngorongoro

Uk. 4

Tahariri/Katuni

Samia kamwe asikubali nchi kurudi gizani

LEO imetimu miezi 41 tangu Samia Suluhu Hassan aapishwe kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Rais Samia alichukua madaraka ya nchi yetu kufuatia kifo cha aliyekuwa mtangulizi wake, John Magufuli, aliyeaga dunia kwa ugonjwa wa moyo.

Wakati wa utawala wa Rais Magufuli, Watanzania na dunia, walishuhudia aina mpya kabisa ya matukio mabaya, yakiwamo ya kuminywa kwa haki za binadamu na kusiginwa kwa Katiba.

Wakati wa Rais Magufuli – kipindi cha zaidi ya miaka sita, Tanzania ikageuka kuwa nchi inayotegemea matamko ya mtu mmoja; rais, kuwa amri na katiba.

Ni katika kipindi cha utawala wake, Tanzania ikarudi kwenye zama za watu wenye mawazo na mitazamo tofauti kuhusu utendaji wa serikali, na hasa taasisi ya urais, kutiwa misukosuko, ikiwamo kutekwa, kupotezwa na zaidi ya hapo.

Tanzania iliyokuwa na jina na sifa nzuri kila pembe ya dunia, kwa mara ya kwanza, chini ya Rais Magufuli, ikaweka rekodi mbaya zaidi kwenye mizania ya kujali na kuheshimu haki za binadamu na hata baadhi ya viongozi wake kutajwa kutatiza haki ya kuishi.

Hata hivyo, mazonge ya utawala wa Rais Magufuli yakaonekana kukoma baada ya ujio wa Rais Samia ambaye aliahidi kwamba ataongoza na kuitumikia Tanzania na watu wake, kwa kufuata misingi ya Katiba na utu.

Hata hivyo, ikiwa imefika miaka mitatu na ushei, Rais Samia akiwa madarakani, nchi inaonekana kurejea kulekule - kwenye wakati wa giza.

Hii inatokana na kuwepo kwa matukio ambayo Watanzania na dunia walikesha wakiomba na kushawishi yasitokee tena, lakini sasa yanaonekana kurejea kwa kasi ileile iliyokuwa ikishuhudiwa wakati wa Magufuli.

Pambazuko linamuomba na kumsihi Rais Samia kukataa kuwa jiwe la chumvi kwa kukemea mambo haya kwani ni chukizo, siyo kwa wanadamu tu, bali hata kwa Mungu.

Ni heri Rais Samia akakemea ‘wahuni’ walioko chini ya taasisi zake, ambao wanaweza kuivuruga nchi na kuirejesha kwenye mazingira ya giza, ambayo wengi bado wanaamini, hayapaswi kushuhudiwa na Watanzania wakati wowote.



Demokrasia...



Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi (katikati) akiongoza kikao cha mashauriano cha vyama vya siasa ambao ni wanachama wa Kituo cha Demokrasia Tanzania (TCD), kushoto ni Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe na Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Emmanuel Nchimbi jijini Dar es Salaam jana. (Picha na CCM)

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon **MKINA**	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter **NYANJE**	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Maregesi **PAUL**	0689 732 325
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth **HOMBO**	0712 792 216
Mkuu wa DTP	:	Yassin **LUPATU**	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia **MFINANGA**	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

Habari

Wamasai ‘wakinukisha’ Ngorongoro



Wakazi wa Ngorongoro wakiwa wamebeba mabango jana wakati wa maandamano yao. (Picha na Mtandao)

Na Mwandishi WETU

MAELFU ya wakazi wa Ngorongoro, mkoani Arusha, wamefanya maandamano ya amani katika maeneo yao kupinga hatua ya kunyimwa haki zao za msingi zikiwemo huduma za kijamii na kupiga kura.

Maandamano hayo yaliyofanyika jana yalisababisha kukwama kwa muda kwa baadhi ya shughuli ikiwemo misafara ya watalii.

Moja kati ya mambo ambayo wananchi hao wanalalamikia ni kitendo cha majina yao kwenye daftari la kudumu la wapiga kura kuhamishwa bila ya wao kupewa taarifa na kupelekwa kwenye kijiji cha Msomera wilayani Muheza, Tanga.

Wananchi hao, ambao wengi wao ni wa kabila la wafugaji la Wamasai, wanataka majina yao yarudishwe kwenye vituo walivyojiandikisha katika eneo la Ngorongoro ili waweze kupiga kura Novemba 27, mwaka huu, kuchagua viongozi wao wa serikali za mitaa.

Mmoja wa waandamanaji hao, aliyejitambulisha kwa jina la Ezekiel ole Mangi, anaonekana katika video iliyorekodiwa wakati wa maandamano hayo na kusambaa katika mitandao ya kijamii, akieleza sababu za wao kuandamana.

“Kuna mambo mengi, yaani ukishaona watu wanaandamana, ujue kuna mambo yameshakuwa magumu kwa sababu kwa muda mrefu sisi wananchi wa Ngorongoro, tumewekewa vikwazo vingi na tumekandamizwa kwa namna nyingi, kiasi kwamba imefika mahali watu hawa wameamua kuingia barabarani kudai haki yao...”

“Kuna mambo ambayo jamii hii imekuwa ikifanyiwa na moja ya vikwazo hivyo ni ukosefu wa huduma za kijamii ambapo ni takribani miaka mitatu sasa, huduma za kijamii hazipo ndani ya Hifadhi ya Mamlaka ya Ngorongoro,” amesema.

Mwananchi huyo anasema wamekuwa wakilipa kodi kama Watanzania wengine, lakini kwa miaka mitatu sasa, hakuna mradi ambao umefanyika katika maeneo yao.

“Kumekuwa na vikwazo vingi ambavyo kimsingi ndivyo vinawakatisha watu tamaa, kumekuwa na vitisho vya aina mbalimbali na kwenye maboma yetu imekuwa kama ni sehemu ya askari wa mamlaka kufanyia doria,” ameongeza.

Mangi anasema hawapingi askari hao kufanya doria, lakini kinachowashangaza ni kwa doria hizo kufanyika kwenye makazi yao, badala ya hifadhini ambako ndiko wanapaswa kuzuia ujangili.

“Shida nyingine ambayo imeleta tatizo zaidi, ni sisi kuondolewa kwenye orodha ya wapiga kura wa nchi hii...”

“Tumejaribu kupiga kelele na kufuatilia kwa taasisi mbalimbali zinazohusika ikiwamo Tume Huru ya Uchaguzi na Tamisemi, lakini kila upande unatupia mpira upande mwingine...”

“Yaani, Tamisemi wanasema wanaohusika ni Tume ya Uchaguzi na wao wanasema anayehusika ni Tamisemi, yaani kila mmoja anarusha mpira kwa mwenzake,” anasikika ole Mangi akisema katika video hiyo.

Pamoja na hayo, anasema baada ya kuona hawana mtu wa kuwasikiliza, wameona njia pekee ni kuitisha maandamano ya amani ili Rais Samia aweze kuwasikiliza na kuwaambia hatma yao.

“Kwa kuwa tumekosa pa kukimbilia, tumeona njia pekee iliyobaki ni kuandamana kwa amani kwa sababu mara kadhaa tumefanya juhudi za kutaka kusikilizwa, ikiwamo kuandika ripoti mbalimbali kwa uongozi wa juu na kuomba kukutana na rais, la-

Inaendelea Uk. 12

Jicho la Tai

Ebo! Wewe Awadh, hebu usituharibie nchi

Na Igo Al

MTANZANIA, anayejitambulisha kuwa mstaafu, anayeishi Mtaa wa Mpakani A, Kijitonyama, Kinondoni, Dar es Salaam, akiitwa Mzee Tai, amemtaka mtu anayeitwa Awadh, aache kuharibu Tanzania.

Kwamba huyo Awadh amesababisha taharuki. Eti ametonesha vidonda na kurejesha makovu kwenye ubichi, wakati maumivu yake yalishaanza kusahaulika.

Kwamba huyo Awadh anataka kuirudisha Tanzania kwenye zama za giza ambazo zilikumbatiwa na kupewa uhai na mwendazake.

Mzee Tai ametoa onyo hilo lenye karipio kali kwa Awadh kwa kuwa anamuona mtu huyo "kutokuwa na nia njema na Tanzania yake.

Mstaafu huyo jana akiwa anazungumza na waandishi wa habari, alisema amelazimika kuwaita kwa kuwa anaona hatari mbele, endapo huyo Awadh ataendelea kuwa na tabia za kifedhuli namna hiyo.

"Mimi juzi nikiwa nakunywa kahawa, nilisikia watu wakimtaja Awadh, kwamba ameleta vurugu kwa kuwakamata kina Freeman, Sugu na kina John wawili, na pia vijana wengine mia tano..."

"Nilipuuza, nikijua huenda ni vijana wavuta bangi wa huko kwa Mtogole, lakini baadaye nikagugundua ni kigogo wa jeshi, hapo ndipo masikio yakanisimama kutaka kujua kulikoni?"

"Wala hakuwa Awadh kutoka kwa Mtogole, kumbe ni kigogo, hapo nikapandwa hasira, iweje huyu mtu aanze tena kuharibu Tanzania na watu wake!"

"Haya mambo ya kukamatana na kutekana, kusumbuana na kulazana Polisi yametoka wapi tena yarabi, au katumwa huyu na wakubwa wake?"

"Lakini hata kama katumwa, yeye hatumii akili za kuzaliwa kama alivyokuwa akisisitiza Jakaya, yule Mkwere wa watu aliyeko Msoga?"

"Huyu Awadh ana akili gani kulazimisha kukamata watu wanaojiandaa kuhudhurua siku muhimu kwa vijana inayoadhimishwa dunia nzima, yeye ni nani? Alilalama Mzee Tai.

Mzee Tai aliwataka waandishi wa habari kufikisha salamu kwa Awadh, kwamba wakati umefika sasa wa kuacha utumishi wa umma na aende akalime karafuu na magimbi.


Mzee Tai akang'aka kwa sauti ya juu, akisema kuwa huyu Awadh anamuharibia mama, kwani anavuruga kabisa maono ya mkuu wa nchi.

Akasema, mama amekuwa akipigania R zake nne, lakini kumbe wapo wasiomuelewa kabisa na sasa wanaingiza tope kwenye uongozi wake.

"Hawa watu wengine sijui wametoka wapi, yaani nchi inasonga mbele, wao wanataka kuirudisha zama za giza, washindwe na walegee kabisa, hatumtaki mtu huyu," alisema mstaafu huyo.

Akiwa na tisheti yake maarufu – ya rangi ya kijani, yenye picha ya mama na maandishi yanayosomeka – "Mitano Tena," Mzee Tai alisema hataki tena kusikia kamatakamata ikirejea na kuharibu sifa za nchi yake na ameahidi kumfikisha salamu hizo mama kwenye vikao vya chama chao hivi karibuni.

Tutumie tafsiri yako ushinde...



Huu ni mchoro wenye maana kubwa. Kila mmoja anaweza kuwa na tafsiri yake, hivyo gazeti la Pambazuko linatafuta tafsiri fupi, inayoelezeka na kufafanua vyema kuliko zote na itachapishwa na gazeti hili kwenye Ukurasa wa 30 toleo linalofuata. Mhusika atatumiwa zawadi – Tuma tafsiri yako kwa simu: 0744 768 263 .

Habari Kuu

Lissu aweka masharti kujiunga CCM

Na Mwandishi WETU

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), bado kina shauku ya kumnasa Tundu Antipas Lissu kuwa mwanachama wake.

Chama hicho tawala, kimekuwa na vikao vingi vya Sekretarieti, vikijadili namna ya kumpata Lissu (pichani), baada ya kufanikiwa kumnasa Mchungaji Peter Simon Msigwa, ambaye alikuwa mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na mjumbe wake wa kamati kuu.

Msigwa, ambaye sasa amekuwa mikutano ya "nyota" kwenye hadhara ya CCM na kuzunguka huku na kule nchi nzima "kuponda Chadema na viongozi wake," ndiye dalali wa kandarasi hiyo ya kumshawishi Lissu kujiunga na CCM.

Taarifa za uhakika ambazo Pambazuko limezipata, zinaeleza kuwa CCM inaamini kwamba kumtumia Mchungaji Msigwa, inaweza kuwa njia rahisi ya kumuona Lissu akiwa amevalia nguo za kijani na kuachana na gwanda za Chadema.

"Unamuona Msigwa anavyopiga kazi, amevaa kijani sasa, na huyu Lissu, nakuhakikishia utamuona hivi karibuni akiwa majukwaani na makomredi wetu; Nchimbi na Makalla, CCM haijawahi kushindwa kitu," ametamba kada wa chama hicho tawala ambaye sasa anaongozana na timu ya sekretarieti kwenye ziara mikoani.

Kada huyo ambaye amekataa kutajwa jina lake amesema "Lissu atakimbia, lakini mwisho tutamnasa," na kwamba iko mipango mikubwa ambayo "hawezi kuchomoa."

Amedai kwamba CCM inaamini kuwa haitafika Aprili, mwaka kesho – 2025, kabla Lissu hajajiunga nao, kwani – anasema; "dalili siyo mbaya hadi sasa."

Kwanini anatumika Msigwa

Taarifa zilizofika kwa Pambazuko zinaeleza kuwa CCM imeamua kumtumia Msigwa iwe rahisi kumpata Lissu, kwani wawili hawa wamekuwa marafiki wakubwa.

Kwamba Lissu na Msigwa, ndani ya Chadema walikuwa kama mapacha, hivyo kuwa rahisi kumshawishi "pacha" wake kuhamia CCM.

Pambazuko linaelezwa kuwa ukaribu wa Lissu na Msigwa nusura ukisambaratishe Chadema, kwani shutuma za Lissu dhidi ya mwenyekiti wa chama hicho kikuu cha upinzani, Freeman Mbowe, chimbuko lake lilikuwa Msigwa.

"Unajua Msigwa alikuwa akimpa makamu mwenyekiti mambo – dhidi ya mwenyekiti, ambayo hayakuwa na ukweli wowote , na bahati mbaya Lissu naye akadhani yana ukweli na kuyabeba kama yalivyo na kuanza kushutumu, hali ilikuwa mbaya sana..."

Endapo mpaka leo Msigwa angekuwa Chadema huenda misingi ya umoja na udugu ndani ya chama chetu ingekuwa imesambaratika, heri alivyoondoka," kimesema chanzo kimoja huku kikiweka msimamo; "usinitaje gazetini."

Mtazamo wa Msigwa

Msigwa amekuwa akimshawishi Lissu hata hadharani, kwamba ni vyema akaachana na "mateso ndani ya Chadema," na kujiunga na CCM ili "akapate raha" anazozipata sasa yeye ndani ya chama hicho tawala.

Alipoulizwa na Pambazuko kuhusu ukweli wa kandarasi yake kwa Lissu ili kujiunga na CCM, Msigwa hakukataa wala kukubali, bali akadai kuwa, akasema anachofahamu yeye ndani ya Chadema kuna mateso na waliomo humo "wanavumilia tu."

Inaendelea Uk. 7

Habari Kuu



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe (kushoto), akijadiliana jambo na Makamu Mwenyekiti, Tundu Lissu (katikati), na Naibu Katibu Mkuu Bara, Salum Mwalimu, wakati wa mkutano na waandishi wa habari, Dar es Salaam mwishoni mwa wiki kuhusu tukio la kukamatwa na kupigwa kwa viongozi na wanachama wa chama hicho jijini Mbeya wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani. (Picha na Fidelis FELIX)

Lissu aweka masharti kujiunga CCM

Inatoka Uk. 6

Msimamo wa Lissu

Pambazuko lilimtafuta Lissu ili aweke wazi endapo yupo tayari kujiunga na chama tawala, CCM ili akapate raha kama anavyoeleza rafiki yake, Msigwa.

Lissu baada ya kupatikana, alisema maneno machache tu kwamba hawezi kujiunga na CCM, kwani anakifahamu vyema chama hicho na kwamba anaweka masharti, endapo ataamua kujiunga huko.

Makamu huyo wa Chadema, akasema, moja ya masharti hayo yataamua endapo atajiunga na CCM, ni kufufuka kwa chama hicho – kwa maana ya "kujikana na kuzaliwa upya."

"Nitajiunga tu na CCM, endapo kitakufa kwanza na kufufuka kikiwa kisafi, kama hilo halifanyiki, basi wasahau, mimi huko siko," amesema Lissu.

Lissu atia nia kuwania urais

Makamu huyo wa Chadema, tayari ameweka nia ya kuwania urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia chama chake katika uchaguzi mkuu unaofanyika mwaka kesho – 2025.

Lissu ameandika barua kwa Katibu Mkuu wa Chadema – na kuiwasilisha Agosti 6, akiomba ridhaa ya chama hicho kupitisha jina lake kuwania nafasi hiyo kubwa kuongoza Tanzania.

Lissu anasema ameandika barua mbili; moja akieleza dhamira yake ya kuomba chama kimteue kuwa mgombea urais wake mwakani ,na ya pili kueleza nia yake ya kutetea nafasi yake ya makamu mwenyekiti katika uchaguzi ndani ya chama.

Lissu anakuwa mwanasiasa wa kwanza mkubwa nchini kutangaza hadharani na wazi kuwa ana nia ya kuwania nafasi hiyo ya juu kabisa ya uongozi nchini.

Wengi wa wanasiasa wanahojiwa na Pambazuko kuhusiana na hilo, wamekuwa wakikwepa kusema wazi kwa kisingizio kuwa wakati muafaka wa kutangaza haujafika.

Inaendelea Uk. 23



Habari

Maono, falsafa za Samia kitanzini

Na Waandishi WETU

MAONO na falsafa ya Rais Samia Suluhu Hassan ya 4R, vimeingia majaribuni kufuatia kuwepo kwa matukio ya kukiukwa kwa haki za binadamu, utu na ustaarabu wa Watanzania.

Ukiacha matukio ya kutekwa kwa watu, Jeshi la Polisi kubebeshwa tuhuma za kuminya utu na demokrasia, kubwa ni tukio la wiki iliyopita jijini Mbeya, ambapo askari wa Jeshi la Polisi walikamata, kupiga na kuwalaza korokoroni timu nzima ya uongozi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema).

Waandishi wa habari waliokuwa wakifuatilia maandalizi ya Chadema, pia "walionja joto ya jiwe" kwa kuteswa na vifaa vyao vya kazi kuharibiwa na polisi.

Katika sakata hilo lililoibuka wakati Polisi ikidai kuwa ilikuwa oparesheni ya kuwazuia wanasiasa hao wa upinzani kufanya kongamano na maandalizi ya maandamano kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani.

Pambazuko limefuatilia maoni ya watu wengi, wakiwamo baadhi ya mabalozi, wamejitokeza kulaani tukio hilo huku wakitaka hatua zinazostahili zichukuliwe dhidi ya wote waliosigina Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuminya ustawi wa demokrasia.

Hata hivyo, pamoja na kulaani, wapo pia watu wanaoeleza kuwa kitendo hicho cha Jeshi la Polisi kukabiliana na viongozi wa Chadema, kisihusishwe na Chama Cha Mapinduzi (CCM), na maono na falsafa ya Rais Samia ya 4R.

Aidha, baadhi ya watu wanasema kilichofanywa na Polisi ni suala la utekelezaji wa sheria hiyohiyo ya kuruhusu kuwepo maandamano, hivyo suala hilo halipaswi kuhusishwa na siasa.

Operesheni hiyo dhidi ya viongozi wa Chadema waliokuwa wanafanya maandalizi ya kongamano hilo iliongozwa na Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Awadhi Haji.

Baadhi ya viongozi wa Chadema waliopigwa na kujeruhiwa wakati wa operesheni hiyo ni makamu mwenyekiti, Tundu Lissu, katibu



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Dorothy Semu.

wake mkuu, John Mnyika, Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi (almaarufu Sugu) pamoja na viongozi wa Baraza la Vijana (Bavicha).

Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe na Mwenyekiti wa Bavicha, John Pambalu, walikamatwa na kusafirishwa kutoka Mbeya hadi Dar es Salaam, ingawa wao hawakupata vipigo.

Wadau wa siasa, viongozi wa dini na watu wa kada mbalimbali, walipaza sauti kuonyesha wasiwasi wao na hofu ya kutekelezwa falsafa ya Rais Samia juu ya ustahimilivu, maridhiano, mabadiliko na kujenga taifa jipya.

Chama cha ACT-Wazalendo ambacho kilitoa taarifa kwa vyombo vya habari kulaani kitendo cha Polisi kupiga wanasiasa waliokuwa wanatekeleza wajibu wao bila kuvunja sheria.

"Vitendo hivyo, vinafufua hofu ya kurejeshwa kwa mazingira kandamizi kwa vyama vya siasa vya upinzani kufanya shughuli zao kwa uhuru na pia tukio hilo na mengine yanayofanywa na dola, yanakinzana na R4 za Rais Samia," linasomeka tamko hilo lililosainiwa na kiongozi wa chama hicho, Dorothy Semu.

Inaendelea Uk. 14

Mezani kwa Chahali

Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com



Chadema wanaweza kuvumilia hadi lini?



Viongozi waandamizi wa Chadema, Godbless Lema (kushoto) akiwa na Patrick Ole Sosopi. (Picha na Fidelis Felix)

NIANZE kwa kutoa pole kwa baadhi ya viongozi na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), waliokamatwa na kudaiwa kupigwa na polisi kufuatia zuio dhidi ya chama hicho kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani huko Mbeya.

Huu utamaduni wa kukamata-kamata na kupigapiga wapinzani na wale wenye mawazo mbadala dhidi ya serikali, ulikuwa umeanza kusahaulika, lakini sasa inaonekana unarejea kwa kasi.

Kuna mambo kadhaa ambayo yangeweza kabisa kuepusha kadhia hiyo.

Kwanza, Jeshi la Polisi halikupaswa kuwazuwia viongozi na wafuasi wa Chadema kufanya maadhimisho hayo mkoani Mbeya na popote pale nchini Tanzania, kwa sababu hiyo ni haki ya kikatiba.

Lakini kinachosikitisha zaidi, wakati polisi wakiwazuwia Chadema kufanya shughuli hiyo, zilionekana picha kutoka sehemu mbalimbali nchini ambapo vijana wa CCM walikuwa wakifanya hichohicho ambacho Chadema walizuiwa kukifanya, huku polisi wakitoa ulinzi.

Hata hivyo, hili siyo la kushangaza kwa sababu yayumkinika kutanabaisha kwamba tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi mwaka 1992, Jeshi la Polisi limeendelea kuwachukulia viongozi na wafuasi wa vyama vya upinzani kama wahalifu.

Ukweli mchungu kuhusu hili ni kwamba licha ya Tanzania yetu kutimiza miaka 32 tangu mfumo wa vyama vingi uruhusiwe, kwa kiasi kikubwa vyombo vyetu vya dola bado vina upeo wa zama za chama kimoja.

Na hili linachangia mno vyombo hivyo vya dola kuona shughuli za vyama vya upinzani kuwa ni haramu ilhali za CCM pekee ndizo halali.

Laiti polisi wetu wangetumia busara, ingewezekana kabisa kuzuia shughuli za Chadema pasipo haja ya kuwakamata wala kuwapiga.

Pongezi za dhati ziwaendee viongozi wa Chadema kwa kutowahamasisha wafuasi wao kukaidi amri ya Polisi, jambo ambalo lingeweza kusababisha madhara makubwa.

Na kwa hakika moja ya sababu zinazosababisha wananchi kukaidi amri ni pamoja na ukandamizwaji wa haki zao waziwazi.

Kadhalika, ni rahisi kwa wanaokandamizwa kuamua kwamba “hata tukitii amri tutaendelea kuonewa tu, kwahiyo bora tukaidi amri na watufanye chochote wanachotaka kutufanya.”

Na uthibitisho ni kwamba hata baada ya viongozi wa Chadema na wafuasi wao kutii maagizo ya Polisi, waliishia kukamatwa na kupigwa ilhali hawakuwa na hatia yoyote.

Kwa upande mwingine, japo viongozi wa Chadema walitumia busara kutohamasisha wafuasi wao kupambana na Polisi, swali linabaki kuwa je chama hicho kitaendelea kuvumilia uonevu huo hadi lini?

Kwa sababu moja ya athari ya kuvumilia ni kujengeka dhana kuwa “kama hawawezi kutetea haki zao wenyewe watawezaje kutetea haki za Watanzania?”

https://instagram.com/evarist_chahali

Tafakuri ya Bagonza

Utukufu wa mihimili na unazi wa vyama vyetu

Na Dkt. Benson BAGONZA

TAIFA letu hivi sasa linaongozwa na pande mbili kubwa; mihimili mitatu ya dola na upande wa pili ni vyama vya siasa.

Kwenye mihimili kuna msisitizo wa "utukufu" wa mihimili ambao siyo mara zote unatokana na usahihi wa kanuni zake. Yaani hata pale kanuni zinazoweza kuonekana za ovyo, zinategemewa zilinde utukufu wa mhimili!

Kwenye vyama, hivi sasa kumetawala unazi au uchawa ambao umekuwa bora kuliko usahihi wa itikadi za vyama na ushirikishwaji wa umma.

Anayeumia katika pande zote ni "uhuru wa dhamiri" kwa waliomo ndani ya mihimili na ndani ya vyama. Kwamba; mtu mzima na akili yake, aweke rehani uhuru wake na dhamiri yake ili kutumikia utukufu wa kanuni na sera zinazolinda chombo bila kulinda utu wa mtu.

Ukiona hivyo, ujue kuna mdudu anaitafuna mihimili na vyama vyetu. Kwa uzoefu, mdudu huyo ni rushwa. Sumu ya mdudu huyu inaua dhamiri, uhuru, haki, uadilifu, na uzalendo.

Sumu hii haiishii kwenye mihimili na vyama. Inaenea hadi patakatifu pa watakatifu (Dini), kwenye vyombo vya habari, kwenye vyombo vyetu nyeti vinavyolinda watu, mali na mipaka yetu.

Aweza kunywa sumu mtu mmoja kwenye taasisi, na wote mliomo mkaonekana mmekunywa sumu hiyo.

Rushwa inashambulia midomo na kuifanya ipoteze uwezo wa kuisema. Baadaye inashambulia uhuru wa aliyekula sumu na kumfanya mpweke katikati ya umati.

Kinachofuata ni upofu. Akiona madai ya haki huyaita majungu au fitna. Yuko tayari kumwita mkewe ni mpinzani kwa kuwa katamka neno "haki."

Katika mihimili yote na vyama vyetu, watu wakweli ni wachache. Ni wapweke, na ni hatari kwa maisha yao wenyewe.

Lakini, hawahawa ndio hushikilia uhai na heshima ya mihimili na vyama hivyo. Uwepo wao hujenga matumaini kuwa ipo siku uhuru na haki vitapata nafasi. Wakiondoka, mihimili na vyama hubakia kuwa mapango ya wanyang'anyi.

Kwa bahati mbaya; kuna ushirikiano wa wababe katika mihimili na katika vyama bila kujali itikadi.

Lakini hakuna uhusiano wala ushirikiano wa watu waadilifu katika mihimili yote na vyama vyote. Wana wa giza wana akili katika mambo yao kuliko wana wa nuru.

Kamwe asikudanganye mtu; kuna mashetani katika kila chombo. Pia kuna malaika kila kila chombo.

Ushetani wa mtu waweza kuichafua taasisi na umalaika mtu waweza kuiokoa taasisi. Tufanye nini?

Mosi, malaika wasiogope mateso. Hofu ni sumu ya malaika. Wakiishinda rushwa, waishinde hofu pia.

Pia, hakuna mwisho mwema kwa uovu wowote. Ikiwa uhalifu wa mtu binafsi una mwisho mbaya, hata uovu wa mhimili na unazi wa chama vina mwisho mbaya. Serikali ina mkono mrefu; Mungu anamiliki mikono ya serikali.



Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



Hoja Yangu

Na Rashid MTAGALUKA

Polisi wanamharibia sifa Samia, akemee

KWA mara ya kwanza tangu nchi yetu irejee kwenye mfumo wa vyama vingi vya siasa miaka 32 iliyopita, hakujawahi kutokea Jeshi la Polisi kukamata wafuwasi wa chama cha upinzani kwa idadi kubwa kama ilivyotokea wiki iliyopita!

Tena kwa kuongezea ni kwamba, historia haijawahi pia kushuhudia Polisi wakifanya 'kufuru' ya kuwakamata viongozi wote wa chama kwa ngazi ya kitaifa kama ilivyotokea huko Mbeya. Hii ni hujuma!

Kwa maneno yake mwenyewe, Kamishna wa Oparesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi Tanzania, Awadhi Haji alisema Agosti 11, mwaka huu, alisema kuwa walikamata watu 375 wakiwemo Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Tundu Lissu.

Wengine waliowakamata siku hiyo kwa mujibu wa Kamanda Haji ni pamoja na Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika, Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa, Joseph Mbilinyi almaarufu Sugu, Katibu Mwenezi wa Baraza la Vijana (Bavicha) Taifa, Twaha Mwaipaya na Makamu Mwenyekiti wa Bavicha, Mozza Ally.

Katika hali isiyo ya kawaida na ambayo imewastua wapenda demokrasia wengi, ni Jeshi hilo kupitia kwa Kamanda Haji, kujisifu mbele ya vyombo vya habari vya kitaifa na kimataifa kwamba, Agosti 12 walikamata wafuwasi wengine 145 wa Chadema, wakiwemo viongozi wa ngazi ya juu wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Kauli hii ya Kamanda Haji kwa hakika inamharibia sana Rais Samia Suluhu Hassan katika siasa za kitaifa na kimataifa. Hatua hii ya Polisi haipaswi kuungwa mkono wala kuchekelewa.

Jeshi la Polisi limeamua sasa kuhujumu juhudi za Rais Samia na kuvuruga falsafa ya mkuu wa nchi ya "R-4" za Maridhiano, Ustaimilivu, Mabadiliko na Ujenzi Mpya.

Nasema wamekusudia kumuhujumu Rais Samia kwa sababu hakuna kati ya viongozi wa Polisi asiyejua dhamira ya kiongozi mkuu wa nchi yetu juu ya kuleta mtangamano wa kisiasa tangu aingie madarakani.

Kama hoja ni ya uvunjifu wa amani, kwanini hatukusikia Kamanda Haji akihimiza kukamatwa kwa mwenyekiti wa UV-CCM Mkoa wa Kagera Faris Burhani aliyesema Aprili 16, mwaka huu kuwa, "CCM inapoteza wapinzani?" Akimaanisha kuminya haki ya kuishi.

Endapo Polisi wangekuwa wanafanya kazi zao kwa weledi, kamwe kusingekuwa na chuki dhidi ya jeshi hilo. Lakini wao wenyewe wamepandikiza chuki hizo kwa kuwa ni kinara wa kuminya haki za binadamu na kuwa chombo cha kuonea na kutesa.

Ni vyema Polisi sasa wajitafakari na kuacha kuharibu mikakati ya Rais Samia kujenga Tanzania yenye umoja, udugu na maendeleo ya pamoja, ikiwa watakaidi, basi akemee na kuchukua hatua.

Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com



Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika

Habari

Wamasai ‘wakinukisha’ Ngorongoro

Inatoka Uk. 4

kini imeshindikana...”

“Kwa kuwa hayo yameshindikana, tumeona njia pekee iliyobaki ni kuandamana kwa amani mpaka Rais Samia mwenyewe aje kutusikiliza na kutoa muafaka, kwani ndiye mwenye uwezo wa kutoa muafaka wa Ngorongoro...”

“Pia akija itakuwa ni pamoja na sisi kujua kama tunabaki hapa ama aamue anavyotaka kwa sababu sisi hatuna nchi au mji mwingine au ardhi nyingine tunayoweza kuishi tofauti na Ngorongoro...”

“Kwa hiyo maandamano yetu ni mpaka tutakaposikilizwa, hayana muda maalum na tunataka Rais Samia ndiye aje atoe tamko,” anasisitiza.

Katika hatua nyingine, mwananchi huyo anawalamu Makamu wa Rais, Dkt. Phillip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambao amesema wamewahi kufika Ngorongoro kwa vipindi tofauti, lakini wakashindwa kutatua malalamiko yao.

Msimamo wa maandamano

Ole Mangi anasema pamoja na uwepo wa vyombo vya ulinzi na usalama katika maandamano yao, hawataweza kusitisha maandamano hayo kwa sababu ni ya amani.

Picha zilizosambaa katika mitandao ya kijamii ziliwaonyesha wananchi hao wakiwa wamebeba mabango yenye ujumbe tofauti, ikiwamo ulioandikwa kwa Kiingereza; ‘it is sad to witness women suffering of oppression led by a woman President’ ikimaanisha kwa Kiswahili - ‘inasikitisha kuona wanawake wakigandamizwa na serikali inayoongozwa na mwanamke;’ ‘kuondolewa Ngorongoro ni mauaji ya kupanga;’ na ‘Nani kapeleka majina yetu Msomera?’

Walalamikia hofu

Katika hatua nyingine, mmoja wa viongozi wa kata za Ngorongoro ambaye hakutaka kutajwa jina lake gezetini, ameliamba Pabazuko kuwa kwa sasa wanaishi kwa hofu kwa kuwa vyombo vya ulinzi vimeshaanza kutoa vitisho dhidi yao.

“Nimekuwa mwoga sana siku hizi katika matamshi yangu na hata matembezi kwa sababu vitisho vimekuwa vingi,” amesema.

Wiki iliyopita Pambazuko liliripoti sintofahau miongoni mwa wakazi wa Ngorongoro ambao majina yao katika daftari la kudumu la wapiga kura yamehamishiwa Msomera.

Ufuatiliaji uliofanywa na Pambazuko kuhusiana na suala hilo haukupata jibu la maana kwa kuwa maofisa kutoka Tamisemi ambayo inasimamia uchaguzi wa serikali na mitaa na wale wa Tume huru ya Uchaguzi (INEC), walitupiana mpira kuhusiana na suala hilo.

Wanazuoni, wanasiasa walonga

Maandamano yaliyofanyika jana yameibua hisia kutoka kwa watu wa kada mbalimbali, wakiwamo wanazuoni na wanasiasa.

Makamu Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu ni mmoja wa waliolizungumzia suala hilo akiilaumu serikali kwa kuwaondolea watu hao huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji na chakula.

“Imewafuta kwa maelfu kwenye daftari la wapiga kura. Licha ya ukatili huu wananchi hawa wamekataa kuondoka kwenye eneo lao. Mimi nawaunga mkono,” anasema Lissu. Prof Issa Shivji akiandika kupitia mtandao wa kijamii anasema: Wakazi wa Ngorongoro na Loliondo, hususan jamii za wafugaji, hawawezi kuondolea kutoka ardhi yao bila kufuata taratibu za kisheria na kwa sababu mahsusi ambayo lazima ijulikane na kujadiliwa hadharani.”

Mamlaka ya Ngorongoro yanena

Baada ya kusambaa kwa picha jongefu za maandamano ya Wamasai na kuonekana kuwepo kwa misururu ya magari ya watalii yakiwa yamesimama, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA), jana ilitoa taarifa kwa umma kuihakikishia kuwa shughuli za utalii zinaendelea kama kawaida.

Taarifa hiyo iliyoandikwa kwa Kiingereza na kusainiwa na kaimu meneja wake wa uhusiano wa umma, Hamis Dambaya ilikiri kuwepo kwa maandamano hayo na kwamba hali ya usalama imedhibitiwa.

Sehemu ya taarifa hiyo inaishukuru serikali kwa kuhakikisha kuwa usalama ndani ya eneo la Ngorongoro unaimarishwa.

Dambaya katika taarifa hiyo anawahakikishia watalii wanaotarajiwa kutembelea vivutio ndani ya hifadhi hiyo kuwa “hakuna tishio lolote la usalama.”

“Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro inawahakikishia watalii wote wenye ratiba za kutembelea Ngorongoro, wasiwe na hofu, kwani serikali iko macho kulinda usalama wao,” inasomeka sehemu ya taarifa hiyo.

Kona ya Dkt. Bisimba



Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA

Haki, utawala wa sheria visipotunzwa, amani itatoweka

KILA wakati ninapoitafakari nchi yetu ninapatwa na maswali mengi. Tunaitwa jamhuri ikimanisha kuwa wananchi ndio msingi wa uongozi au utawala wa nchi.

Lakini je, tunayoyafanya yanakisi hilo? Tuna Katiba ambayo pamoja na kuwa ina changamoto zake nyingi, lakini ina mifumo inayowezesha kuendelea katika utawala wa sheria na kuzingatia haki tulizo nazo tukiwa binadamu.

Tulipitia kipindi kilichotujaribu kuona Katiba inavyochezewa na kuonekana kuwa ni 'kijitabu tu' kwa maana ya kuwa mtawala angeweza kutoa amri ikafuatwa hata kama iko kinyume cha Katiba na sheria za nchi.

Na jambo kubwa tulilojifunza ni ustahimilivu wa Watanzania kwamba watu wanaweza kutekwa wakapotea na watu wasifanye chochote zaidi ya manung'uniko ya chini chini.

Watu wanaondolewa kwenye makazi yao bila fidia, wanabaki kuiomba serikali iwafikirie na wapo watu waliouawa kabisa na miili yao kukutwa kwenye mifuko ufukweni mwa bahari, lakini hakuna anayeonekana kuguswa.

Kila mtu anakuwa kama amepigwa ganzi.

Wengi tulidhani hayo yamepita na awamu ya tano, maana awamu ya sita ilipoingia tukaaminishwa kuwa tunaanza ukurasa mpya na tunaijenga upya nchi kwa kufuata falsafa ya R4 alizoziibua Rais Samia Hassan Suluhu; Reconciliation (Maridhiano), Resilience (Ustahimilivu), Reforms (Mabadiliko) na Rebuilding (kujenga upya).

Hizi 'R' 4 zilionekana kuleta matumaini mapya hasa kwa jinsi Rais Samia alivyozielezea, akisisitiza angetamani kuiona nchi yenye umoja bila kujali tofauti zilizopo za itikadi, dini na hata kabila.

Pia tulimsikia mwenyekiti wa chama kikuu cha upinzani; Chadema, Freeman Mbowe, akiweka mkazo kuwa hategemei yaliyopita katika awamu ile, yakiwamo ya wapinzani kukamatwa, kushitakwia kwa makosa yasielezeka ya ugaidi, yatajirudia.

Tulianza kuona mabadiliko kiasi kwa vyama vya upinzani kurudi katika hali ya kuweza kufanya mikutano hata maandamano. Watu kupotea au kuuawa kukakoma. Lakini, sasa kidogo kidogo tukaanza kusikia watu wakiwa wamepotea au wamechukuliwa na watu waliosadikika kuwa polisi na hatimaye wasionekane.



Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe.

Nchi ilipata taharuki kubwa kwa kilichotokea kwa viongozi na wanachama wa Chadema waliotaka kufanya kongamano ya Siku ya Kimataifa ya Vijana huko Mbeya, Jumatatu iliyopita.

Pamoja na kongamano hilo kupigwa marufuku, lakini tumeshuhudia watu wakikamatwa, kuwekwa ndani, kupigwa na kuumizwa, huku mali zikiharibiwa.

Hata Mbowe, ambaye aliungana na Rais Samia kusisitiza R4, naye alikuwa miongoni mwa watu waliokumbwa na sekeseke hilo la Jeshi la Polisi.

Kwa mgeni aliyeona jinsi wanachama wa Chadema walivyondewa na Polisi, asingeamini kuwa wale ni wanachama wa chama cha siasa na siyo wahalifu sugu.

Ni kwa nini haya yanajirudia tena? Ndio swali kubwa lililonijia. Hivi Rais Samia ana taarifa au ndiye aliyeamuru haya?

Je, Mkuu wa Jeshi la Polisi ndiye aliyeamuru haya? Na kama waliamuru haya, nia hasa ni nini katikati ya nia iliyoonekana ya kujenga nchi kwa umoja na kufuata utawala wa sheria na haki za binadamu?

Iwapo Rais Samia hakuruhusu haya, kwa nini hatuoni hatua yoyote iliyochukuliwa dhidi ya aliyeongoza operesheni ile?

Huu uvumilivu tulionao Watanzania ambao hautokani na ile falsafa ya Rais Samia, ukijaribiwa sana iko siku nchi itaangukia kwenye wimbi kubwa la machafuko yasiyohimilika.

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.

Habari

Maono, falsafa za Samia kitanzini

Inatoka Uk. 8

Hashimu Rungwe

mwenyekiti wa CHAUMA, Hashim Rungwe, aliiambia Pambazuko kwa njia ya simu kwamba walichofanyiwa Chadema ulikuwa ni uonevu ambao hauwezi kuungwa mkono na mtu yeyote.

"Kama Chadema walikuwa na makosa, polisi walitakiwa wawadhibiti mapema, kwani wana intelijensia ya kutosha ambayo inaweza kujua mambo yoyote ya uhalifu.

"Wamewatia hasara Chadema, wamewaumiza na kuwahaharibia mali, hawakufanyiwa jambo zuri kabisa, nalaani kabisa jambo hilo.

"Kwa hiyo, hata hizo 4R za Mama Samia zimeharibiwa kabisa ingawa kwa upande mwingine, nasema hizo 4R ni hadaa tu kwani kama ni suala la sisi wanasiasa kufanya mikutano ya kisiasa, ni suala la kikatiba, siyo hisani hata kidogo," amesema Rungwe.

Absalom Kibanda

Mwandishi wa habari ambaye pia ni Mwenyekiti (mstaafu) wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Absalom Kibanda, alionyesha kutoridhishwa na tukio hilo na kutoa tahadhari kupitia mtandao wake wa kijamii.

"Sisi tuliokuwa tukijifaharisha na falsafa ya 4R za Rais Samia, tumeumbuliwa na fedheha ya matukio ya viongozi wakuu wa Chadema kukamatwa na kufanyiwa ukatili usiomithirika kule Mbeya, tujitafakari," alisema Kibanda kwa kifupi.

Dkt. Kahangwa

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dkt. George Kahangwa, alieleza kusikitishwa kwa walichofanyiwa makada wa Chadema, akisema hakutarajia hayo yatokee katika utawala wa awamu ya Rais Samia.

"Kwa kweli kilichotokea Mbeya kinatisha sana, hasa ukizingatia kwamba kinatokea katika nchi inayoamini katika umoja, uhuru na hizo tunu tunaziimba pia katika wimbo wa taifa.

"Sasa watu wanapokamatwa na kupigwa kiasi hicho unajiuliza juu ya matumizi ya hekima katika vyombo vyetu vya dola; sasa hiyo ndiyo hekima tunayoimba Watanzania?"



Profesa Safari



Absalom Kibanda

"Haya mambo hatukuyatarajia yatokee katika utawala huu kwa sababu tayari nchi hii ilishapitia machungu mengi,"alisema Dkt. Kahangwa, akizungumza na Pambazuko.

Kutokana na hilo, msomi huyo alishauri kuwa ni wakati sasa kwa wenye mamlaka, kuliangalia upya Jeshi la Polisi na kwamba linatakiwa kuundwa upya ili lirudi katika misingi ya kuwalinda raia na mali zao.

Ubalozi wa Marekani

Katika taarifa yake, Ubalozi wa Marekani nchini Tanzania umeonyesha masikitiko yake kwa Polisi kutumia nguvu kubwa kuwadhibiti wanasiasa kiasi cha kuwamuza.

"Tumestushwa na taarifa za kuaminika kwamba, polisi walitumia nguvu kupita kiasi wakati wa kuwakamata viongozi wa Chadema, washiriki vijana na waandishi wa habari kabla ya mikusanyiko iliyopangwa kufanyika Mbeya katika kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Vijana.

"Uhuru wa kujieleza, kukusanyika kwa amani na haki ya kupata mchakato wa haki, ni haki za msingi na serikali zote zina jukumu la kudumisha misingi hii ya kidemokrasia.

Profesa Safari

Mwanasheria maarufu nchini, Profesa Abdallah Safari, amelaani tukio hilo na kuwashangaa polisi kwa jinsi walivyoharakisha kuwadhibiti Chadema wakati kwa upande mwingine wameonyesha udhaifu kushughulikia matukio mengine ya uharifu yanayotokea nchini.

"Polisi hawahangaiki na vyama vingine, wao mahangaiko yao ni kupambana na Chadema.

Inaendelea Uk. 15

Maono, falsafa za Samia kitanzini

Inatoka Uk. 14

Yaani, Chadema wanapopanga mambo yao, Jeshi la Polisi liko kinyume, ingawa tulidhani mambo yamebadilika.

"Baada ya kuona kilichotokea Mbeya, tukajua mambo bado ni yaleyale, ni aibu. Huwezi ukawa mbaya moyoni, halafu ukafanya mazuri nje, haiwezekani kwani ubaya ulioko ndani kuna siku utaonekana nje hata kama kuna wakati utajifanya wewe ni mzuri.

"Polisi wanachukua bunduki kubwa kubwa, wanavaa sare zao ili washughulike na vijana wa Chadema wasitimize maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani wakati hayo ni maadhimisho ya kimataifa.

"Linapokuja suala la kukabiliana na uharifu mkubwa mkubwa nchini, hawawezi kutumia bunduki zao kubwa kuwasaidia wananchi na wala hawawezi kutumia bunduki zao kubwa kubwa kuwatafuta waharifu katika nchi yetu."

"Hiyo siyo professionalism (taaluma), watambue Mungu anawaona na kama wanatumwa, huyo anayewatuma naye Mungu anamuona," alisema Profesa Safari katika andiko lake kwa vyombo vya habari.

Wabunge CCM wanena

Wakati hao wakisema hayo, Mbunge wa Mtera, Livingstone Lusinde, alizungumza na Pambazuko na kuwalaumu Chadema kwa kufanya maadhimisho ya siku hiyo ya vijana bila kufuata utaratibu.

"Kwanza kabisa nasema CCM haihusiki na tukio hilo la Mbeya, haihusiki na watu wasiihusishe kabisa..."

"Pia, ieleweke kwamba siku zote za kimataifa zikiwamo siku ya vijana, siku ya wanawake, Siku ya Mtoto wa Afrika na nyinginezo za kimataifa, huadhimishwa kiserikali ambapo mgeni rasmi anakuwa ni kiongozi wa serikali wala siyo kiongozi wa kisiasa kama Lissu..."


"Kwa kuwa Chadema inaonekana hawajui utaratibu wa maadhimisho ya siku hizo, basi kuna haja ya kuwapa elimu ya jinsi ya kuziadhimisha kwa sababu inaonekana hawajui kinachoendelea..."



Balozi wa Marekani, Michael Battle



Mbunge wa Mtera, Livingstone Lusinde



Hashim Rungwe



Dkt. Kahangwa

"Hata hivyo, Chadema wanatakiwa washukuru viongozi wa Mkoa wa Mbeya kwani wamewasaidia kuonekana katika kurasa za mbele za magazeti badala kurasa za nyuma ambako kwa muda mrefu wamekuwa wakiandikwa na vyombo vya habari..."

"Kuhusu 4R za mama, sina tatizo na hilo, zinatekelezwa kwa vitendo na ushahidi wa hilo ni jinsi Watanzania wanavyoshuhudia nchi ikienda mbio kwa maendeleo," alisema Lusinde.

Mbunge wa Mtwara Mjini, Hassan Mtenga (CCM), alisema walichofanya Chadema ni uvunjaji wa sheria na Katiba ya nchi, na kamwe wasitafute visingizio vyovyote.

"Sheria na haki ni mambo mawili tofauti, hawa viongozi wa Chadema walikuwa bungeni, wanaijua Katiba, na hizi sheria wanazijua kwa sababu walishiriki kuzitunga, hivyo wanazivunja makusudi kutafuta huruma kwa watu; tufike mahali tuseme ukweli kwa sababu hata haya maridhiano wanayavunja wenyewe"alisema Mtenga.

Ana kwa Ana

Othman: Katiba ya Jamhuri mtego kwa Muungano



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Na Waandishi Wetu, Zanzibar

KATIKA sehemu hii ya pili ya mahojiano na Pambazuko, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Othman Masoud Othman, anazidi kuelezea mambo anuai kuhusiana na masuala ya kisiasa, kijamii na kiuchumi ambayo yanaikabili serikali hiyo hivi sasa.

Endelea…

Pambazuko: Awali ilidaiwa kuwa watu wanaodai serikali tatu katika Muungano wana lengo la kuuvunja. Baadaye ikaelezwa kuwa mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar ni hatari kuliko wanaodai serikali tatu. Una maoni gani katika hili?

Othman: Tukizungumza hivi vitu viwili, hatutapata hoja ya msingi. Unapolieleza jambo hili ni vyema kwenda ndani zaidi ili kuwawezesha watu kuona tatizo hasa liko wapi.

Tatizo lipo kwenye Katiba ya Muungano na utekelezaji wake.

Tuna serikali mbili na katika serikali hizi mbili, Zanzibar ina mambo mengi ambayo inataka iyaendeshe, serikali ya Muungano ina mambo machache ya Zanzibar na inaendesha mambo mengi ya Tanganyika.

Ukirudi kwenye Katiba ya Muungano, suala la ushuru wa forodha, ushuru wa bidhaa, kodi ya mapato, bandari, mafuta na gesi, simu, usafiri wa anga, usafirishaji kwa njia ya anga, takwimu na leseni za viwanda, haya yote ni mambo ya Muungano.

Lakini, leo ukitazama mapato yanayotokana na TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) yote yanayokusanywa Zanzibar, yanabaki Zanzibar.

Bandari imeelezwa kwenye Katiba kuwa ni suala la Muungano, lakini leo hii Zanzibar inaendesha bandari zake yenyewe.

Zanzibar mafuta wanaagiza wenyewe, wanaweka regulations (kanuni) wenyewe. Sasa hivi tumetangaza tunauza vitalu offshore (baharini) wanaotaka waombe vitalu vya gesi na mafuta, sisi Zanzibar wenyewe.

Sasa kesho akitokea kiongozi wa Muungano ako akasema kwa muda mrefu CCM wamekuwa wakiendesha hii nchi kwa makubaliano yao wenyewe.

Lakini, mimi nimeapa kutetea katiba na kwa mujibu wa Katiba hiyo, suala la ushuru na kodi ni suala la Muungano, bandari ni jambo la Muungano na mafuta na gesi ni jambo la Muungano.


Kwa hiyo, kuanzia tarehe Mosi Julai, mapato yote ya ushuru yaingie kwenye mfuko wa Muungano na bandari tutaleta mtu aje asimamie huko. Vile vitalu tunavirudisha TPDC (Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania) kwa sababu ndilo lenye dhamana ya kusimamia mambo hayo.

Huyu hatakuwa amevunja Katiba lakini kuna serikali ya Zanzibar tena hapo?

Pambazuko: Kwa hiyo Katiba ya Muungano ndiyo hatari zaidi kwa Muungano?

Othman: Ni hatari kubwa zaidi kwa sababu ndio msingi. Ile iliyofanyika Zanzibar 2010 (mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar) ni

Inaendelea Uk. 17



Othman: Katiba ya Jamhuri mtego kwa Muungano

Inatoka Uk. 16

jambo la kisheria.

Ni haki yake Zanzibar kufanya hivyo kwa sababu ni sehemu ya Muungano na hakuna mahali Tanganyika imefutwa na hakuna mahali Zanzibar imefutwa.

Ibara ya nne ya Katiba ya Muungano, inaweka msingi wa kisheria wa hilo jambo, kwamba tuna Muungano wa nchi mbili; kuna Zanzibar, kuna Tanganyika na kuna mambo ya Muungano.

Yaani tuna two states (mataifa mawili) na tuna three jurisdictions (maeneo matatu ya utawala).

Huu ndio msingi wa Muungano ambao upo kwenye hati ya Muungano.

Jambo ambalo Katiba imelionea haya kusema wazi wazi ni kuwa huu ni Muungano wa nchi mbili na hizi nchi mbili bado zipo.

Na hii ni aina ya Muungano ambao unapatikana sehemu nyingi duniani. Ukisoma Katiba ya Uswisi, wana majimbo kama 26, ambayo ni sawa na nchi.

Tofauti ni kuwa katika katiba yao, yale majimbo yote yametajwa kwenye katiba kama sehemu ya Swiss Federation (Muungano wa Uswisi).

Katiba ya Marekani vilevile inalinda uwepo wa majimbo.

Sasa sisi Katiba yetu imeona haya kutaja kuwa Muungano huu ni wa Tanganyika na Zanzibar na kwamba hizi ni states (taifa) na si nations (nchi).

Watu wanashindwa kutofautisha state (taifa) na sovereignty (himaya). Sovereignty inaweza kubaki sehemu moja, lakini hiyo haizuii states kuendelea kuwa na mamlaka yake ya ndani, lakini tu zisiingilie mamlaka ya himaya.

Na sisi hapa tunapawa kuwa na states ambazo zina mamlaka yake, lakini sovereignty inabaki sehemu moja ya United Republic of Tanzania (Jamhuri ya Muungano wa Tanzania).

Lakini, mimi nadhani badala ya kulaumiana na kuona nani ni hatari, turudi tutengeneze misingi ya Muungano wetu.

Leo tumeacha Katiba. Ikitokea mtu anatekeleza Katiba hapa anaonekana hafai.

Akitokea kweli mtu akaisimamia Katiba ya Muungano, nchi hii itakuwa na crisis (mgogoro).

Pambazuko: Kwa hiyo mabadiliko ya 10 ya Katiba ya Zanzibar yamekuja kujibu hilo?

Othman: Ndiyo as a state. Kwa kuwa Katiba ya Muungano haikutoa jibu, Zanzibar ikaamua kujieleza kuwa sisi ni nchi within a state.

Mabadiliko ya kumi ya Katiba ya Zanzibar ni suala la Zanzibar kutekeleza majukumu yake as a state (kama taifa).

Ni lazima ijitambulishe kama state kwa sababu kusema tu sehemu ya Jamhuri ya Muungano haitoshi.

Inabidi kueleza sehemu kama nani, kama kitongoji? Kama Kata? Kama Mkoa?

Katiba ya Muungano haitoji jibu hilo na Katiba ya Zanzibar ikasema sisi tutaoa jibu, ikasema sisi ni nchi kwa maana ya within a state (ndani ya Taifa).

Pambazuko: Umezungumzia umuhimu wa kuwa na uchaguzi huru na wa haki. Je, kutokuwa na uchaguzi wa aina hiyo ni matokeo ya udhaifu wa kimfumo na kisheria au ni udhaifu tu wa watu waliopewa dhamana ya kuongoza taasisi za uchaguzi?

Inaendelea Uk. 18

Ana kwa Ana

Othman: Katiba ya Jamhuri mtego kwa Muungano

Inatoka Uk. 17

Othman: Nadhani ni yote mawili, lakini lipi kubwa zaidi.

Ukitazama Tume ya Uchaguzi ilivyo, ina uwezo wa kufanya uchaguzi ukawa huru.

Ukitazama mahakama, kwa jinsi ilivyoundwa, ingawa majaji wanateuliwa na rais, lakini wanalindwa na Katiba, kwa hiyo wana uwezo wa kufanya kazi kwa uhuru.

Tatizo linakuja kutokana na tabia na mwenendo na uendeshaji wa wale wanaosimamia taasisi hizi.

Mathalan, suala lipo mahakamani, kiongozi anamwita jaji anamwambia suala hili toa uamuzi huu. Kuna mwingine anaweza kutekeleza maagizo hayo na mwingine atasema hapana.

Tatizo kubwa lipo kwa viongozi wanaosimamia haya.

Ukitazama Katiba ya Marekani kwa mfano, haina sifa ya mtu kuwa jaji, lakini hawajawahi kuchagua scientist (mwasayansi) au daktari wa binadamu akaenda kuwa jaji.

Huku kwetu sisi tumebainisha sifa za jaji awe hivi, awe hivi lakini wanachaguliwa watu hopeless (wasiofaa).

Kuna mambo mengi wala mtu ahitaji kuongozwa kwa kuwekewa masharti.

Mfumo huuhuu uliopo, ukipata kiongozi wa kweli, mwenye dhamira ya kufanya uchaguzi wa haki, tutafanya uchaguzi wa haki.

Pambazuko: Mlipoingia kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), mlisema hamfuati vyeo. Lakini wewe ni makamu wa rais na kuna wengine wamepata uwaziri, kwa mwananchi wa kawaida hivyo ni vyeo. Unalizungumziaje hili?

Othman: Wala usianze na mimi, uanze huko nyuma. Msingi wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilikuwa ni kuwa tuna tatizo Zanzibar, hivyo tutengeneze mazingira ya kutatua tatizo hilo.

Na hili lilianza kitambo tulipoona kuwa siasa zetu hazipo sawa. Tutafute jambo gani tutoke hapa?

Msingi wa SUK si kwamba ndio mmefika, ni fursa ya kutengeneza tiba ya tatizo linalowakabili.

Si kuwa mkitengeneza SUK, na nyie mmo ndio tatizo limeisha, la hasha.

Hii ni safari, lakini tumekuwa tukizunguka hatuendi mbele. Dhamira ya SUK si kwamba muingie ndio jambo limeisha.

Lazima tukubali kuwa sisi Zanzibar uchumi wetu ni uchumi wa huduma, unaohitaji watu waje, muuze huduma nje, mnahitaji uwekezaji mkubwa.

Kwa mtu ambaye ana fedha katika ulimwengu wa sasa, kabla hajaja kuwekeza Zanzibar, anafanya due diligence (upimaji) ili kuepuka political risk (hatari za kisiasa).

Akija akikuta kuna SUK, sisi tunaona kuwa SUK ni fahari, lakini yeye anaona hawa hawapo sawa. SUK ni ant-business (kikwazo kwa biashara), mtu yeyote mwenye hela akisikia mna SUK anajua hawa watu hawajakaa sawasawa.

SUK maana yake mna kiraka, mmechanikiwa na nguo, mmeweka kiraka ili mkanunue nguo nyingine.

SUK ni suala la mpito, si mila kuwa mnatembea na kiraka. Hadi lini? Mkifika mkaona kuwa SUK ndio suluhisho hamtatui tatizo. Kwa hiyo SUK si vyeo, ni suluhisho la mpito tu.

Inaendelea Uk. 19



Mwalimu Julius Nyerere akichanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar ili kuziunganisha nchi hizo mwaka 1964. (Picha na Maktaba)

Othman: Katiba ya Jamhuri mtego kwa Muungano

Inatoka Uk. 18

Pambazuko: Lakini suala hili la SUK limeshaingizwa kwenye Katiba, hauoni kuwa kulitoa humo itakuwa ni ngumu?

Othman: Katiba si ilitengenezwa 2010 ikaingizwa? Mnaweza kufika mahali mmeshatengeneza misingi ya kuendesha nchi ambayo haihitaji SUK.

Kimsingi, SUK ni mpaka mpate watu viongozi walio sawasawa, msipokuwa na watu wa aina hiyo, ni mfumo mgumu sana.

Ni kitu kinachohitaji maelewano ya kudumu. Kwa hiyo tukifikia hatua tumesimamisha misingi, linaondolewa tu kwenye Katiba.

Pambazuko: Hivi kuna migongano ya kisera mnapotekeleza mambo mbalimbali huko serikalini maana serikali inaundwa na CCM na ACT-Wazalendo?

Othman: Migongano ipo. Ni lazima iwepo maana unajua, ni kwamba wananchi waelewe kuwa kuendesha serikali kwa kutumia zaidi ya chama kimoja si jambo geni duniani.

Kuna nchi kubwa zilizoendelea zina serikali zinazoendeshwa na chama zaidi ya kimoja.

Uswisi, Ujerumani, hata Israel ambao wana magomvi ya kila siku, Afrika Kusini wameingia DA na ANC, si jambo geni.

Lakini, misingi yake ni kuwa mkubaliane kwenye mambo ya msingi kama walivyofanya DA na ANC.

Kila chama kinapoingia kwenye serikali ya aina hii, inabidi kikubali kuwa sehemu ya sera zitakazokubalika kuendesha serikali hata kama sera hizo si zake.

Kama hukubaliani hilo, serikali ya umoja haiwezi kufanya kazi.

Hii ni kwa sababu kama chama hakiamini katika sera zake, basi kisingeingia kwenye uchaguzi, wameingia kwa sababu wanaamini wana mambo ya kuyatekeleza na watu wanayapenda.

Sasa wanapopata nafasi ya kuongoza serikali ni lazima watataka zile sera zao ndizo zitumike kuendesha serikali au ziwe ehemu ya sera zinazoendesha serikali.

Kuna mambo hapa kwetu watu wanakubali sera za kwetu kuliko za CCM. Na si kwamba hamuwezi kufanya pamoja.

Pambazuko: Wanachama wengi wa ACT-Wazalendo wametoka kwenye chama cha CUF ambacho kinahusishwa sana na siasa za historia. Vipi kuna athari zozote kwa ACT-Wazalendo na siasa hizi za kihistoria?

Othman: Hata wakati ule ilikuwa ikitumika kama manipulation (hila) za kisiasa. Kwamba CUF ndio ilikuwa Hizbu na CCM ndio iliyokuwa ASP.

Lakini ukiangalia vyema, namba tu zinaonyesha kuwa haikuwa hivyo. Kwa mfano mdogo tu, uchaguzi wa mwisho uliofanyika kabla ya Mapinduzi, Julai 1963 ukitazama chama cha Afro Shirazi ambao ndio hao wanaohusishwa na CCM, kwa upande wa Pemba chama kile kilipata kura 33,850, ambazo zilikuwa ni asilimia 44 ya kura zote za Pemba. Ikavishinda vyama vingine kwa mbali sana.

Lakini zilipokuja siasa hizi, ikaonekana labda Pemba yote ni wapinzani, lakini wanasahau kuwa ASP ilipata kura nyingi ikavishinda vyote kule.

Kwa maana hiyo, ilikuwa ni stronghold (ngome) ya ASP na baadaye ikaja kuwa stronghold ya upinzani.

Lakini ukiangalia mimi leo siijui Hizbu na nimepindukia miaka 60. Sasa kama mimi siijui Hizbu, vipi kwa mtoto wangu ambaye ni mpiga kura ambaye hakuwepo wakati huo atajua relevance (maana) ya Hizbu?

Tatizo ni kuwa watu tunashikilia sana stori za zamani. Sasa stori zote za zamani zimekwisha. Ni wakati wa kujenga stori mpya ambazo ni maendeleo ya nchi hii.


Hata mtu akitaka kuitumia stori hiyo haitamsaidia, itakuwa inampotezea muda tu.

Pambazuko: Kuna jambo jingine lolote ambalo ungependa kulisema kwa umma wa Watanzania?

Inaendelea Uk. 20

Ana kwa Ana

Othman: Katiba ya Jamhuri mtego kwa Muungano



Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi (kulia), akiwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman.

Inatoka Uk. 19

Othman: Nadhani watu hatujawasaidia vya kutosha. Kwamba mwelekeo, hasa wa Zanzibar, hapa tulipo tupo katika hali mbaya kiuchumi.

Mathalan, tazama katika mwaka huu wa fedha, makusanyo yote ya fedha yatafikia shilingi trilioni 1.5 na kati ya hizo, shilingi bilioni 900 zinakwenda kulipa mishahara.

Tutabakiwa na bilioni 600. Ukisoma tena bajeti yetu utakuta kwamba bilioni 300 tunakwenda kulipa madeni, kwa hiyo tutabakiwa na bilioni 300 ndiyo ya kuendeshea serikali. Pengine labda tuende tukope.

Lakini, unakopa kulingana na uwezo wako. Ukikopa zaidi maana yake utakuja kuchukua tena hiyo bilioni 300 iliyobakia kulipa madeni.

Hili si suala la siasa. Ni lazima kama Zanzibar tutoke hapa.

Ukitulinganisha na wenzetu wadogo wadogo kama Seychelles, Maldives na Mauritius, wametupita mbali sana.

Mfano mzuri sisi na Mauritius, ukitazama land size (ukubwa wa ardhi) wao ni 2,000 square kilometers (kilometa za mraba) sisi ni 2,600 tupo kubwa kidogo, lakini ukitaza geographical position (eneo la kijiografia) na mambo mengine, sisi tulipaswa kuwa mbali sana, lakini ukitaza bajeti yao wao ni trillion 13.

Lakini kinachoumiza zaidi ni kuwa kati ya hizo trillion 13, za kwao za ndani ni trilioni 11.6, ni za makusanyo ya ndani, wanakopa trilioni 1.4 pekee.

Ukianza kuilinganisha hiyo na sisi Zanziabar hivi kweli sisi ni wa kupitwa na Mauritius takribani mara kumi?

Kuna magic (uchawi) gani? Resources (rasilimali) za ajabu, hawana mafuta, hawana madini, mbona wanatupita?

Alipata kusema Margaret Thatcher kuwa maendeleo baina nchi na nchi hayatofautishwi na resources. Tofauti inakuja namna mnavyoendesha mambo yenu - mfumo wa kisiasa, governance (utawala), maadili, maono, jinsi mnavyoendesha nchi hilo ndilo litaleta tofauti.

Ninachosema ni kwamba inafaa hili tulione kwa upana wake. Wengi wanapozungumza Zanzibar wanazungumza misuguano ya kisiasa, lakini tuna tatizo la msingi ambalo kama hatutasimama kulitatua, mimi naona tunakokwenda kunatisha sana.

Beyond us (mbele yetu) tunawatengenezea vijana tatizo kubwa sana. Natamani watu wasio wanasiasa wakalieleza hili maana tukilisema wanasiasa, tunaonekana kama unapiga siasa.

Tungekuwa na think tank (makundi ya ubunifu) na klabu za waandishi wa habari, nadhani haya ni mambo ya msingi kuyazungumza.



Naibu Rais Kenya awa mwiba Serikali ya Ruto

Na Julius MKAMBI, Nairobi

HISTORIA ni kama inajirudia kwani kile kilichomkuta William Ruto wa Kenya wakati akiwa Naibu Rais chini ya utawala wa Rais Uhuru Kenyatta, ndicho sasa kinamzonga Naibu Rais Rigathi Gachagua.

Ruto alipinga tukio la March 9, 2018 lililobatizwa 'handshake' baada ya Rais Kenyatta kuibuka na hadharani na hasimu wake kisiasa, Raila Odinga, na kuhutubia taifa wakitangaza kuzika tofauti zao ili kufanya kazi pamoja kwa ajili ya ustawi wa nchi.

Baadaye viongozi hawa walikuja na rasimu iliyofahamika kama Building Bridges Initiative (BBI) ikilenga kufanya marekebisho kwenye Katiba iliyopitishwa mwaka 2010.

Hata hivyo, Ruto alikuwa miongoni mwa viongozi wakuu serikalini na wanasiasa waliopinga BBI na ushindi wao ulipatikana baada ya Mahakama ya Juu (Supreme Court) kutupilia mbali BBI kwa misingi kwamba ilikiuka sheria.

Ruto alionekana mpinzani ndani ya serikali huku kukiwa na tetesi ya serikali kusuka njama ya kuleta hoja bungeni ya kutokuwa na imani na naibu rais, lakini changamoto ikawa ni kupatikana idadi ya wabunge watakaofanikisha kupitishwa kwa hoja hiyo ikizingatia Ruto tayari alifanikiwa kuvuta baadhi ya wabunge na wanasiasa upande wake.

Tetesi kama hizo za hoja kuletwa bungeni kumtimua Gachagua zimeibuka tena na haishangazi zimeshika kasi kipindi ambacho Rais Ruto amefungua milango ya kufanya kazi na kiongozi wa upinzani, Raila baada ya kuteua viongozi wanne waandamizi wa Chama cha Orange Democratic Movement (ODM) kwenye baraza jipya la mawaziri.

Gachagua mara kadhaa amesikika akisema hakutakuwa na 'handshake' kati ya Ruto na Raila na kwamba "alikuwa ametega mitego Ikulu ya kumnasa Raila" endapo atajaribu kuingia Ikulu.

Kama hiyo haitoshi, kauli ya Gachagua kwamba Rais Ruto hawezi kuwapa nafasi wapinzani, kwani nchi siyo kampuni yake binafsi.

Kauli ya Gachagua iliwakera wapinzani wakisema wametengwa wakati wao pia wanalipa kodi wa Kenya, hivyo wanapaswa kuwa sehemu ya uamuzi na hatma ya nchi yao.

Ukaribu wa Rais Ruto na Raila, unaonekana kumpa wakati mgumu Gachagua ambaye amekuwa akitajwa kuwa anajipanga kumrithi bosi wake Ruto pindi atakapomaliza kipindi chake cha uongozi.

Inavyoelezwa ni kwamba, Gachagua hakupendezwa na uamuzi wa kuwapa nafasi za uongozi wapinzani ndani ya serikali.

Ni kutokana na msimamo wake huo, wapo wanaodai kuwa zipo tetesi za kuondolewa madarakani na hoja hiyo ambayo haijathibitishwa , inachochewa zaidi na namna anavyopigia debe maendeleo kupelekewa eneo la Mlima Kenya anapotoka yeye, huku akisema hawezi kuomba msamaha kwa kupenda watu wake.

Wanaoshinikiza Gachagua kuondolewa ofisini wanadai mienendo yake haiendani na hadhi ya ofisi anayoshikilia wakisisitiza kuwa

Inaendelea Uk. 22



Naibu Rais wa Kenya, Rigathi Gachagua

Kenya

Naibu Rais Kenya awa mwiba...



Rais wa Kenya, William Ruto

Inatoka Uk. 21

yeye ni kiongozi wa taifa na siyo mbunge huku pia wakimshutumu kueneza siasa za ukabila kinyume na msimamo wa Rais Ruto anayewataka wanasiasa kuacha siasa za kikabila.

Mbunge wa Kitui ya Kati, Makali Mulu, amesema baadhi ya wabunge kutoka eneo la Mlima Kenya wamechukua hatua kali kuhusu hoja ya kumuondoa Gachagua.

"Panapofuka moshi, pana moto na kile kinachoendelea ni kwamba Naibu Rais anahitaji kujiandaa kwa sababu kuna taratibu zinaendelea chini chini za kukusanya saini ili kumuondoa Gachagua kwenye nafasi yake," amesema Mbunge Mulu.

Naibu Rais Gachagua mwenyewe alisema anajua mpango unaosukwa kumuondoa madarakani na kuongeza kinachochochea jambo hilo ni msimamo wake thabiti kuhusu umoja wa eneo la Mlima Kenya, ikiwemo kupigania haki zao serikalini.

Je, hii kupigania haki za eneo la Mlima Kenya serikalini ndiyo inaleta mtafaruku na bosi wake Ruto? Au ni jambo jingine likiwamo la kuwepo kwa taarida "za ndani ya Ikulu" zinadai wabunge 21 na waziri moja ndiyo wanaosuka mpango wa kusukuma hoja ya kumuondoa Gachagua.

Wabunge hao na waziri, wote kutoka Mlima Kenya wanadai Naibu Rais Gachagua anamhujumu Rais Ruto na amekuwa akieneza siasa za mgawanyiko wa kikabila.

Aidha, wanasema Rais Ruto alichukizwa na taiba ya naibu wake ambayo ni pamoja na kutoa madai yasiyofaa ya uteuzi serikalini.

Gachagua pia amekuwa akinyooshewa kidole kwamba alikuwa anapinga Muswada wa Fedha 2024 ambao hatimaye ulichochea vijana wa Gen Z kuandamana.

Hata hivyo, wapo baadhi ya wabunge na wanasiasa wanaodai ,uwa watasimama na Gachagua, wakisisitiza hawataweka saini au kupiga kura kuondolewa kwa naibu huyo wa rais kwa sababu hii ni mbinu ya kumtisha.

Mbunge wa Embakasi Kaskazini, James Gakuya, amesema sasa ni wakati wa kuacha kutumia hoja ya kumuondoa Gachagua, kwani inaweza kuwa ni njia ya kumnyamazisha.

Mwakilishi wa Wanawake Kaunti ya Kirinyaga, Njeri Maina, amemtaka Rais Ruto kumlinda naibu wake kutokana na vita vya kisiasa ndani ya chama tawala.

Aliyekuwa Makamu wa Rais, Kalonzo Musyoka, naye anatajwa kuvaa viatu vya Raila kuongoza upinzani hususan baada ya Raila kushirikiana na Rais Ruto.

Kalonzo amesema kuwa viongozi wa vyama vya upinzani hawatakubali Gachagua kuondolewa, na kwama endapo hilo litafanikiwa, basi Rais Ruto naye pia aondoke.

Ibara ya 150 ya Katiba ya Kenya inaeleza sababu za kumwondoa naibu rais, ikiwa ni pamoja na kutokuwa na uwezo wa kimwili au kiakili au ukiukaji mkubwa wa masharti ya kikatiba.

Swali sasa linabaki kuwa - je, hoja ya kumuondoa ofisini Gachagua itatinga bungeni? Na kama ikitokea imeingia, naibu rais huyo anayo idadi ya kutosha ya wabunge kupindua meza na kuhakikisha anasalia kwenye madaraka?

Je wajua



Kulala kwa saa nyingi au kwa muda mfupi vinaweza kuchangia mtu kunenepa kupita kiasi. Utafiti umegundua kuwa usingizi usio mzuri unaweka mtu kwenye hatari ya kunenepa kupita kiasi. Muda unaopendekezwa na wataalamu ni kulala saa nane, sio zaidi wala pungufu.



'Mongoose' ni miongoni mwa wanyama ambao hata wakigongwa na nyoka hawafi, licha ya umbo lake kuwa dogo lakini anaweza kupambana na nyoka yoyote.

Lissu aweka masharti...

Inatoka Uk. 7

Hatua hii ya Lissu inakuja siku chache tu tangu Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Boniface Mwabukusi, kuhoji kwa nini Chadema kisimtangaze rasmi Lissu kuwa mgombea wake wa urais.

Mwabukusi anasema siyo siri kuwa Lissu ni mmoja wa wanasiasa wanaofahamika nchini na nje ya nchi na pia mwenye mvuto kwa wapigakura wengi kutokana na ujasiri na utendaji wake kisiasa.

Wakati Lissu akitangaza nia yake hiyo hadharani wanasiasa wengi wameamua kubaki na dhamira zao vifuani.

CCM hali ikoje?

Ndani ya CCM, ingawa kumekuwa na msukumo wa kutaka mwenyekiti mwake wa sasa, Rais Samia Suluhu Hassan awanie nafasi hiyo, lakini siyo Samia mwenyewe au chama chake kinachobainisha hilo waziwazi.

Hata hivyo, hilo halijawazuia baadhi ya wanachama ndani ya chama hicho, wakiwamo waandamizi kuonyesha dhamira kuwa Rais Samia ndiye atakuwa mshika bendera wa chama hicho kwenye uchaguzi wa rais mwakani.

Yametolewa hadi mapendekezo ndani ya chama kuwa ichapishwe fomu moja tu ya mwanachama anayetaka kuomba kuteuliwa kuwa mgombea urais na fomu hiyo iwe ni kwa ajili ya Rais Samia.

Msukumo huo haupo tu ndani ya chama, kwani hivi karibuni kundi la wahandisi walijitokeza hadharani na kusema kuwa wamenunua helikopta ambayo watamkabidhi Rais Samia kwa ajili ya kufanyia kampeni wakati wa uchaguzi mkuu mwakani.

Makundi mengine mengi ya watu nayo yametangaza kuchangishana fedha kwa ajili ya kupata fedha zitakazomwezesha Rais Samia kulipia fomu ya kuomba kuteuliwa kuwa mgombea urais kupitia chama chake, CCM.

Pambazuko lilipatia

Kuondoka kwa Msigwa Chadema kujiunga na CCM kuliandikwa na gazeti la Pambazuko na baada ya siku nne, kweli kiongozi huyo alitambulishwa kujiunga na chama hicho tawala.

Alipoulizwa na Pambazuko kwamba zipo taarifa kuwa atajiunga na CCM, Msigwa aling'aka, huku akilifokea gazeti hili, kwamba limepata wapi habari hizo, lakini baada ya siku nne, akaonekana akipokea kadi ya CCM na kuvalishwa nguo za rangi ya kijani, maarufu kwa utambulisho wa chama hicho tawala.

Msigwa akikataa na kukemea Pambazuko, lakini baada ya siku nne, akajiunga na chama hicho tawala

Mtoto wa Mvuvi



Na Maregesi PAUL

OSHA sasa ijitangaze ili waajiri, wafanyakazi na wananchi waijue



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa kazi (OSHA), Khadija Mwenda. (Picha na Michuzi Blog)

MWISHONI mwa wiki iliyopita, nilihudhuria semina iliyoandaliwa na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA), jijini Dar es Salaam.

Semina hiyo iliyofunguliwa na Mtendaji Mkuu wa OSHA, Khadija Mwenda, ilihudhuriwa na waandishi wa habari ambao ni wanachama wa Chama cha Waandishi wa Vyombo vya Habari Tanzania (Jowuta).

Nilimsikiliza vyema Mwenda, nikawa macho zaidi kwa Mwanasheria wa OSHA, Rehema Msekwa, nikakaa vizuri kujua alichokuwa akikizungumza Meneja wa Mafunzo na Uhamasishaji, Shaabani Mbaga na pia nilimfuatilia kadiri nilivyoweza, Mkufunzi wa OSHA, Moteswa Meda.

Aidha, naamini kabisa kuwa wanahabari nao waliwaelewa vizuri viongozi hao kwa kuwa walitaka kujua zaidi ya majukumu ya OSHA.

Hakika, Mwenda na timu yake walijitahidi kuwaeleza wanahabari walichokuwa wamewaitia ili iwe rahisi kwao kufikisha ujumbe kwa waajiri na wafanyakazi katika sehemu mbalimbali nchini.

Wakati wa kipindi cha maswali na majibu, ndipo niligundua kwamba baadhi ya wanahabari walioshiriki mafunzo hayo hawakuijua OSHA kabla, licha ya taasisi hiyo kuwa moja ya taasisi muhimu za serikali.

Kwa kifupi, waandishi walifurahia mada muhimu zilizokuwa zikiwasilishwa, huku wengi tukionekana kuwa tulikuwa “weupe” sana kuhusu masuala ya afya na uhusiano na afya ya watendaji.

Wanahabari walishangaa jinsi sumu inavyoweza kuondolewa kwa urahisi mwilini, baada ya mtu kula au kuinywa, walikuwa wakishangaa jinsi ya kuwatambua nyoka wenye sumu kali na wasiokuwa na sumu, pia walifundishwa njia za kunusuru maisha ya mtu aliyepatwa na shambulio la moyo.

Waandishi wa habari ambao ni muhimu kufikisha ujumbe kwa jamii, walikuwa weupe katika elimu iliyowasilishwa kwao, ingawa OSHA ipo nchini miaka mingi na ina matawi nchi nzima.

“Kushangaa kwa waandishi wa habari,” maana yake ni kwamba OSHA ambayo ni taasisi ya umma, shughuli zake hazifahamiki sana kwa wananchi.

Kutokana na hali hiyo, OSHA sasa inatakiwa iamke, isilale usingizi, isipoteze muda kwa watendaji wake kukaa ofisini na kupigwa viyoyozi, bali wajipange kuhakikisha inafahamika vyema kwa umma.

Maofisa wa OSHA wasitumie muda mwingi kuwasiliana na wenzao katika makundi ya WhatsApp, yafaa sasa watembelee maeneo yote ya kazi ili kutatua changamoto zinazohusu ofisi hizo kwa mujibu wa sheria.

Yaani, kama waandishi wa habari hawana uelewa wa kutosha kuhusu OSHA, uwezekano wa waajiri na wafanyakazi nchini kujua mambo muhimu wanayotakiwa kuyafanya ili wasivunje sheria, unakuwa ni mdogo.

Kwa maana hiyo, OSHA, ina wajibu wa kujitangaza na kueleza umma umuhimu wake kwa wafanyakazi na pia inatakiwa iwaeleze waajiri umuhimu wa kusajili maeneo yao ya kazi kama sheria zinavyoelekeza.

Wafanyakazi waonywa kujali zaidi kazi badala ya afya zao

Na Hellen NGOROMERA

WAFANYAKAZI nchini wameaswa kujali zaidi afya zao wanapokuwa kazini, ili kuwaepusha na madhila ya "kujikana."

Kwamba wapo wafanyakazi ambao hujali zaidi kufanya kazi kwa bidii na kwa muda mrefu, lakini wakisahau kutunza afya zao.

Meneja wa Mafunzo na Uhamasishaji wa Wakala wa Usalama na Afya mahali pa Kazi (OSHA), Mhandisi Shaaban Mbaga, alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari ambao ni wanachama wa Chama cha Wafanyakazi wa Vyombo vya Habari (Jowuta).

Alisema kwa kiasi kikubwa wafanyakazi wengi wamekuwa wakijali zaidi kazi kwa kuwa ndio inawaletea kipato, huku wakipuuzia kutunza afya zao.

Hatua hiyo ya kusahau afya zao wanaokuwa kazini kumekuwa kukisababisha majanga mbalimbali ikiwemo kupata ulemavu wa kudumu na hata vifo.

"Wafanyakazi wana wajibu wa kufahamu afya zao kwa kupimwa miili yao mara kwa mara ili kuwaondolea matatizo ya kupata magonjwa hasa ya mshtuko…"



Mwenyekiti wa Jowuta, Mussa Juma

"Dawa nyingi tunazokunywa hovyo zinaweza kutuletea usugu mwilini hivyo tuwe makini nazo," alisema Mhadishi Mbaga.

Alisema ajali nyingi zinawakumba watu wakiwa kazini pamoja na kupata magonjwa mengi yanayosababishwa na kazi nyingi, hivyo wafanyakazi wanapaswa kuchukua tahadhari kwa kuepuka vihatarishi wanapokuwa kazini ili wabaki salama.

Mhandisi huyo alisema ikiwa majanga yatamtokea mfanyakazi atapata athari za kiuchumi ikiwemo kupoteza kazi hivyo kukosa kipato kabisa.

Mbaga alieleza pia kuwa matatizo mengi yanayochangia kuwepo kwa ugonjwa wa afya ya akili yanatokana na mazingira ya kazi, kwani usalama wa mtu unaanzia kwenye akili.

Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa OSHA, Rehema Msekwa, alisema sheria ya usalama mahali pa kazi ilitungwa na Bunge mwaka 2003 kwa lengo la kuweka viwango vya usalama na afya bora maeneo ya kazi ili yawe salama na yenye afya.

Kwa mujibu wa wakili huyo, lengo la sheria hiyo ni kumwezesha mfanyakazi kuwa salama anapokuwa kazini hadi muda wa kumaliza kazi.

"Osha ni taasisi ya serikali iliyoundwa na serikali kwa ajili ya kusimamia usalama na afya mahala pa kazi kwa lengo kuu la kuwalinda wafanyakazi wanapokuwa kazini wasipate majanga yoyote kama ajali, magonjwa kazi na mengine" alisema.

Mwenyekiti wa Jowuta, Mussa Juma, alisema lengo la ofisi yake kuomba kupatiwa mafunzo hayo ni kuwawezesha wanachama wake kufahamu vyema majukumu ya OSHA ili nao wapate nafasi ya kuelimisha vyema jamii.

Habari



Bwawa la Kidunda

Bwawa la Kidunda kuhifadhi maji ya kutumika mwaka Dar es Salaam

Na Mwandishi WETU

SERIKALI imeanza ujenzi wa bwawa kubwa la kuhifadhia maji la Kidunga kwa ajili ya matumizi ya wakazi wa Dar es Salaam kwa gharama ya shilingi bilioni 336.

Ujenzi wa mradi huo ambao hivi sasa inaelezwa kuwa umefikia asilimia takriban 20, unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2026.

Litakapokamilika, bwawa hilo litakuwa na uwezo wa kuhifadhi lita bilioni 190 za maji ya kutumiwa na wakazi wanaofikia milioni saba na ushei.

Kwa kiwango cha hivi sasa cha uzalishaji wa maji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (Dawasa) wa lita milioni 534 kwa siku, maji hayo ya Kidunda yanaiwezesha mamlaka hiyo kuzalisha maji kwa siku 355, takribani mwaka mmoja, kama vyanzo vingine vyote havitatoa maji.

Taarifa iliyotolewa kwa wahariri na Dawasa hivi karibuni, ilieleza kuwa pamoja na kuhifadhi maji, mradi huo unaojengwa na Kampuni ya Sinohydro Corporation ya China, pia utazalisha megawati 20 za umeme.

“Kiasi cha umeme huu kitatumika kuendesha mradi na kiasi kingine kitaingizwa kwenye gridi ya taifa,” alisema Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Dawasa, Mkama Bwire.

Wakati huohuo, Dawasa imewakaribisha wafanyabiashara kutoka sekta binafsi kushirikiana nayo katika nyanja mbalimbali zinazohusu usambazaji wa huduma ya maji.

Bwire alibainisha kuwa moja ya maeneo hayo ni uzalishaji na usambazaji wa mita za maji za malipo ya kabla.

“Hili eneo la mita za kulipia kabla ni moja ya maeneo ambayo sekta binafsi inaweza kushirikiana na sisi kulitekeleza...”

“Ni eneo linalohitaji uwekezaji mkubwa, kwani meta hizi ni za gharama kidogo. Tunaweza kuingia makubaliano na wafanyabiashara , aidha kuzalisha mita hizi au kuzisambaza kwa wateja,” alisema Bwire.

Akifafanua kuhusu mita hizo, Bwire alisema sasa hivi zimeshaanza kufungwa kwa baadhi ya wateja kwa ajili ya majaribio na majaribio hayo yatakapokamilika na mita hizo kupasishwa, zitaanza kusambazwa kwa wateja wote.

Wakati huohuo, Bwire alisema katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, Dawasa imepata mafanikio makubwa ikiwemo kuongeza uwezo wake wa uzalishaji maji kutoka lita milioni 520 kwa siku hadi lita milioni 534 kwa siku sawa na ongezeko la lita milioni 14.6 kwa siku.

Changamoto

Hata hivyo, Bwire alibainisha kuwa licha ya kazi kubwa inayofanyika kuimarisha upatikanaji wa maji katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na baadhi ya maeneo ya mkoa wa Morogoro ambayo wanaihudunia, mamlaka inakabiliwa na changamoto kadhaa kubwa ikiwa ni mabadiliko ya tabia nchi ambayo yanakwaza upatikanaji wa maji ya kutosha.

Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Bwire alibainisha kuwa Dawasa imeongeza juhudi katika kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutunza mazingira.



Mafuta ya Uganda sasa kupitia Bandari Dar

Na Mwandshi WETU

KUTOKANA na kuwepo maboresho makubwa ya kimfumo na utendaji katika Bandari ya Dar es Salaam, Serikali ya Uganda imeamua kuanza kuitumia kusafirisha mafuta yake.

Uamuzi wa Uganda kuitumia Bandari ya Dar es Salaam na "kuikimbia" Bandari ya Mombasa, Kenya, umefikiwa baada ya Shirika la Mafuta la Uganda (UNOC) kufanya tathmini na kujihakikishia ufanisi uliolivutia.

Sasa UNOC itakuwa ikipokea na kusafirisha bidhaa za mafuta kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

Bandari ya Dar es Salaam, ambayo ni kitovu cha uchumi wa Tanzania, imekuwa katika maboresho makubwa ambayo sasa yanaiwezesha kupokea meli kubwa zaidi, kupungua kwa muda wa kupakia na kupakua mizigo na mfumo wa kisasa wa kusambaza taarifa.

Maboresho hayo yamefanikiwa kwa kuwepo uwekezaji mkubwa unaofanywa na Kampuni ya DP World ya falme za Kiarabu.

UNOC imekuwa ikitumia zaidi Bandari ya Mombasa, Kenya kuchukua bidhaa hizo na kusafirishwa kwa kutumia Shirika la Bomba la Kenya (KPC).

"Uganda imepanga kusafirisha takriban lita milioni 36 za mafuta kila mwezi, kupitia Bandari ya Dar es Salaam, baada ya kuridhishwa na maboresho yanayofanywa katika kitovu hicho cha usafiri wa majini kwa nchi za Afika Mashariki," amesema Mkurugenzi Mtendaji wa UNOC, Proscovia Nabbanja.

Hata hivyo, UNOC imesema kiasi hicho kinatarajiwa kuongezeka kadri siku zinavyosonga.

Sehemu ya kwanza ya shehena ya mafuta tayari ilisafirishwa wiki iliyopita kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuelekea Uganda.

Katika shehena hiyo, jumla ya lita milioni 18 za mafuta (karibu sawa na kutumia malori 520 kusafirisha bidhaa hiyo) ilipakiwa.

Makubaliano kati ya Bandari ya Dar es Salaam na Shirika la Mafuta la Uganda (UNOC) yalifanyika Mei 24 hadi 25, 2024 wakati wa Mkutano wa Pili wa Biashara kati ya Uganda na Tanzania uliofanyika Dar es Salaam.

Katika mkutano huo, nchi hizo mbili zilikubaliana kuboresha njia za usafirishaji wa mafuta na bidhaa nyingine kupitia Bandari ya Dar es Salaam badala ya Mombasa, Kenya.

Uamuzi huu ulifikiwa kutokana na mabadiliko ya kiufundi na gharama katika usafirishaji wa mafuta kupitia Bandari ya Mombasa, na hivyo Uganda ikaamua kuongeza matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam kama njia mbadala ya kusafirisha bidhaa za mafuta yake.

Katika mkutano huo, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati wa Tanzania, Dkt. Doto Biteko alisema lengo la makubaliano ya mkutano huo ni kuimarisha uhusiano wa kiuchumi kwa nchi hizo mbili, ambazo ni "ndugu, siyo kwa kufanya baishara pekee, bali hata maeneo mengine yakiwamo ya kijamii."

Riwaya

Viaticum-2

Sakramenti ya Mwisho



Rais wa zamani wa Cuba, Fidel Castro

Na Mchungaji Godwin Chilewa, Texas. Marekani

WIKI iliyopita tuliona namna Eddy alivyopata hisia kwamba majambazi waliokuwa wakiua watu walikuwa nia ya kutuma ujumbe kwa serikali.

Endelea kuona nini kitatokea...

Wakati akiendelea kutafakari habari hiyo, mlango wa ofisi yake ukafunguliwa. Stella, katibu muhtasi wake akaingia huku akitabasamu.

Stella ni msichana wa kupendeza sana. Mrefu kiasi cha futi tano inchi sita, mwembamba, mwenye umbo la kuvutia. Ngozi yake laini ya maji ya kunde ilimfanya aonekane kama mwana mitindo.

Nywele zake ndefu, nyeusi tii, aliweza kuzichana kwa mtindo wowote autakao. Leo hii alizibana kama mkia wa farasi.

Macho yake makubwa yaliyolegea kama binti aliyekula kungu, yalivutia kiasi cha kuweza kumfanya bosi yeyote mwenye uhanga kumpa talaka mkewe ili aweze kuishi na binti huyu.

Lakini siyo Eddy, mtu mwenye kujiheshimu na kufuata maadili ya kazi. Asubuhi hii Stella alivalia sketi fupi ya rangi nyeusi, blauzi ya mikono mifupi yenye rangi ya poda na viatu vyeusi vyenye kisigino kirefu.

"Samahani bosi" Stella aliomba radhi huku akitembea taratibu kuelekea mezani kwa Eddy.

"Bila samahani Stella. Vipi, kwema?

"Kuna barua hii nimeipokea sasa hivi kutoka kwa mfanyakazi wa posta, inaonekana ni ya haraka," alisema huku akimpa bahasha kubwa ya rangi nyeupe iliyotengenezwa kwa karatasi ngumu.

Eddy akaipokea na kuiangalia kwa makini. Upande wa mbele yalichapwa maandishi makubwa ya rangi ya bluu yaliyosomeka Expedited Mail Service. Pembeni uligongwa muhuri wa rangi nyekundu ulioonesha barua hiyo ilitumwa kutoka Jiji la Mwanza.

"Ahsante Stella. Tafadhali keti nikupe maagizo kabla sijatoka humu ofisini," alimwambia huku akijiweka vizuri kwenye kiti alichokalia nyuma ya meza kubwa iliyotengenezwa kwa mbao za mninga.

Stella akatupa macho yake kwa chati kuangalia mezani.

Hakukuwa na kitu chochote kipya. Katikati ya meza kulikuwa na 'skrini' mbili za kompyuta ya mezani aina ya Dell zilizounganishwa katika mtandao mmoja.

Pembeni ililala kompyuta mpakato aina ya Apple MacBook Air. Upande wa kushoto yalipangwa mafaili kadhaa yanayosubiri kushughulikiwa.

Kulia yaliwekwa magazeti ya siku hiyo, na mafaili mengine yaliyo katika hatua ya mwisho ya uchunguzi. Nyuma ya kiti alichokalia Eddy kulikuwa na 'rafu' kubwa iliyopangwa vitabu vya aina na lugha mbalimbali

Kwa muda wa miaka mitatu na nusu Stella amekuwa akifanya kazi ofisini kwa Eddy akiwa katibu muhtasi wake.

Shughuli yao kubwa ni uandishi wa habari za kipelelezi na uchapishaji wa gazeti la wiki liitwalo Mizani. Ofisi yao iko katikati ya Jiji la Dar es Salaam kwenye jengo la IPS lililo mkabala na sanamu ya askari

Gazeti hili hutoka kila siku ya Jumapili likiwa limesheheni habari za kipelelezi hususan

Inaendelea Uk. 29

Riwaya

Viaticum-2

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

zinazohusu matukio na kashfa za viongozi wa serikali na wafanyabiashara wakubwa, taarifa za uchunguzi wa kesi za jinai zilizotelekezwa au kushindikana.

Pia gazeti hilo huandika makala mbalimbali za kuelimisha jamii kuhusu haki na wajibu wao kisheria. Jina 'Mizani' lilitokana na kauli mbiu 'Mizani ya haki' iliyokuwa maarufu kwa wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu.

Mwanzilishi wa gazeti hili alikuwa marehemu inspekta Godfrey Hatibu, ofisa mstaafu wa Jeshi la Polisi. Huyu aliliendesha kwa miaka miwili tu kabla ya kuuawa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana.

Kifo chake kilileta taharuki kubwa miongoni mwa wananchi.

Wengi waliamini kifo chake kilitokana na njama zilizopangwa na viongozi wa juu serikalini waliochukizwa na jitihada zake za kupinga maovu.

Viongozi hao walikanusha uvumi huo kwa nguvu na kusisitiza kwamba marehemu inspekta Hatibu aliuawa kwa njama zilizopangwa na wafanyabiashara wa dawa za kulevya aliokuwa akiwaandika mara kwa mara gazetini na kuchochea kukamatwa kwao.

Viongozi wa chama tawala wao walimlaumu mkuu wa Jeshi la Polisi kwa kutompa ulinzi inspekta Hatibu, hasa baada ya gazeti lake kuandika habari zilizosaidia kusambaratishwa kwa mtandao mkubwa wa dawa za kulevya nchini.

Kauli hiyo ilileta mkanganyiko mkubwa kwa sababu ilipingana na taarifa iliyotolewa na jeshi hilo ambayo ilidai marehemu inspekta Hatibu aliuawa na majambazi waliovamia nyumbani kwake kwa lengo la kupora fedha na vitu vingine vya thamani.

Baada ya kifo cha inspekta Hatibu, ndipo Eddy aliponunua hisa zote za kampuni ya Mizani. Uamuzi huo ulisukumwa kwa kiasi kikubwa



na mtafaruku uliojitokeza kwenye familia kuhusu mrithi halali wa mali za marehemu.

Kwa bahati mbaya inspekta Hatibu hakuwa na mke wala mtoto anayetambulika kisheria, jambo lililoongeza ugumu wa mambo.

Ili kuepusha mgogoro, mahakama iliteua msimamizi wa mirathi na kuamuru mali zote ziuzwe ili kila anayestahili apewe haki yake.

Kwa kuwa wakati huo Eddy ndiye aliyekuwa mhariri mkuu, mkurugenzi wa fedha na mmiliki wa asilimia 25 ya hisa za kampuni, akaona bora anunue hisa zilizobaki kuliko kuacha zinunuliwe na mtu asiyejua malengo ya msingi ya gazeti la Mizani.

Ndipo akachukua mkopo benki na kulipia asilimia 75 ya hisa zilizokuwa mikononi mwa marehemu inspekta Hatibu.

Kwa bahati mbaya, kifo cha inspekata Hatibu kilirudisha nyuma sana umaarufu wa Mizani. Baadhi ya waandishi nguli, wapelelezi maarufu, na wataalam wengine walikimbia kwa kudhani bila inspekta Hatibu hakuna lolote la maana linaloweza kufanyika.

Hili halikumshangaza Eddy, kwani wafanyakazi wengi walimuona inspekta Hatibu kama Fidel Castro wa Cuba, pasipo yeye hakuna mwingine.

Ni katika kipindi hiki, Eddy alipouona umuhimu wa Stella. Binti wa watu alimsaidia kwa kila hali kuhakikisha Mizani halipotezi umaarufu wake.

Stella alifanya kazi kwa bidii, mara nyingine mpaka usiku wa manane, tena bila kudai malipo ya muda wa ziada. Baada ya miezi sita ya ubunifu na jitihada kubwa umaarufu wa Mizani ukarudi na kuongezeka mara dufu.

Ndipo sasa waandishi wengine wakaanza kukimbizana kutaka kujiunga na Mizani.

Itaendelea wiki ijayo...

Habari katika picha



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na viongozi mbalimbali katika Mkutano wa 44 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuia ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) uliofanyika kwenye Jengo la Bunge la Zimbabwe Jijini Harare tarehe 17 Agosti, 2024. (Picha zote na Ikulu)









Na Hellen NGOROMERA



Hakuna asiyefanya makosa kwenye ndoa

KATIKA maisha ya ndoa, mume na mke wana wajibu wa kuelewana, kushirikiana na kusaidiana ili kuijenga na kustawisha familia.

Wanandoa kutendeana mambo hayo kunaweza pia kuwafanya wajisikie fahari na kuimarisha nyumba yao kuwa bora, yenye upendo, kusikilizana na mafanikio.

Upendo na kusikilizana kati ya wanandoa hao husaidia watoto wao pia kujisikia amani.

Wiki iliyopita nilizungumza namna matendo maovu ya mke au mume yanavyoweza kufifisha, kuharibu au kuvunja ndoa au uhusiano.

Nilieleza kwamba mwanaume kwa kiasi kikubwa anaweza kuwa chanzo cha kuharibu ndoa, nikatoa mifano.

Moja ya mifano ni kuwa ndoa nyingi huvunjika kutokana na wawili hao kushindwa kuvumiliana na kuishi kwa kuwekeana visasi na mambo yanayofanana na hayo.

Mada hiyo ilimfanya msomaji mmoja kunitumia ujumbe mfupi kwenye simu yangu na kuniandikia hivi; “nimesoma makala yako ya masuala ya uhusiano, lakini unaegemea upande mmoja tu. Je, hakuna wanawake wenye matatizo pia?

“Ukiona mwanaume hatendi sawa kwa mkewe, ujue kuna mahali kakwazika...”

“Mwanaume huwa anaumiza kichwa kutafuta pesa kwa ajili ya familia, mwanamke anaweza kutumia bila kufikiria hiyo pesa imepatikanaje, na kwa maumivu gani, ukim-bajetia (ukimpangia bajeti) mwanamke anakuona bahili wakati wewe unajua ulivyopata.”

Ujumbe huu ulinitafakarisha sana na nimeona bora nitumie uwanja huu huujadili kidogo.

Ndoa nyingi hukumbwa na matatizo mbalimbali, lakini mengi hutofautiana kutokana na uzito wa tatizo.

Unaweza kukuta ndoa ina mgogoro fulani kutokana na kuwepo sintofahamu kati ya mke na mume.

Wakati mwingine unaweza kukuta mke hatimizi wajibu wake kwa mumewe kama ambavyo msomaji wangu amegusia, hivyo kufanya mume kushindwa kuvumilia hali hiyo.

Mwanamke anaweza kutotimiza wajibu wake kwa mumewe na hiyo huenda inatokana na kukerwa na mambo kadha wa kadha, lakini kiuhalisia mwanamke hapaswi kulipa kisasi hata kama amekerwa.

Mwanamke anapaswa kuwa mstari wa mbele kumtii na kumheshimu mumewe kwa kila hali; hata Maandiko Matakatifu yanafundisha hivyo.

Mwanamke anapaswa kuwa mfano bora katika maisha ya familia.

Wakati mwingine mwanamke anaweza kuwa chanzo cha migogoro ndani ya familia na kuonyesha visa, visasi, au mambo mengine kutokana na kukerwa na mambo anayofanyiwa na mumewe.

Jambo hilo huleta migongano na uvunjifu wa amani na wakati mwingine husababisha ndoa kuvunjika.

Kuna wakati mwanaume anaweza kushindwa kutimiza wajibu kwa mkewe au familia kutokana na kuchukizwa na matendo ya mkewe, kama vile kutokuwa mwaminifu na mtiifu.

Kikubwa kinachotakiwa katika uhusiano au ndoa ni kuvumiliana kwa mambo yanayoweza kusawazishika, kuheshimiana na kupendana.

Hayo yote yakifanyika yatawezesha wana ndoa kuishi kwa amani, upendo na furaha.

Hivyo, ni kweli kuwa matatizo katika ndoa yanaweza kusababishwa na yeyote; mume au mke. Kinachotakiwa, mmoja anaposababisha matatizo hayo, mwingine awe mtulivu, kisha wote washauriane kwa lengo la kurekebisha tatizo hilo.

Tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0754 88 67 49.

Mitindo & Urembo

Na Agatha Charles

Namna unavyoweza kujipambanua kupitia mavazi

MAVAZI humwelezea mtu namna alivyo.

Wapo wanaovaa wasiweze kuvutia kutokana na mtu kutokujua kanuni za kila vazi na maana ya kuvaliwa na wakati gani avae, vazi la aina gani.

Leo nakukumbusha kuchagua namna unavyotaka watu wakuchukulie kulingana na mavazi yako.

Hapa nazungumzia wale ambao wanavaa mavazi yao lakini hawastui, yaani hawapati ule mvuto wa vazi husika.

Kumbuka kuwa kupendeza kunamwongezea mhusika ujasiri mbele za watu.

Mambo ya kuzingatia;

*Unataka kutambulikaje; wapo wanaotambulika kwa kuvaa suti, kaunda suti, gauni tu, sketi na blauzi au koti au kuchanganya. Tafuta kinachokufaa kikutambulishe.

*Kuwa na chaguo bora; inabidi ujijue kuwa ni kipi ukivaa kinakukaa vizuri na unakuwa huru. Ukijijua, basi jitahidi kupita humohumo kwa kubadili mitindo na rangi za vazi lako husika.

* Pitia nguo zako; uwe na tabia ya kukagua nguo zako na kupunguza zisizofaa. Usiache kabati lijae nguo ambazo huzitumii. Utaonekana una nguo nyingi lakini hazina maana.

Unapokagua na kupunguza nguo usizovaa, unapata nafasi ya kuongezea zinazohitajika tu.

* Usisahau viatu; viatu vikiwa bora vinakubeba kwa kiasi kikubwa kimuonekano, hata kama nguo ulizovaa siyo nzuri sana.





Tusisahau sunscreen

JUA kali linaharibu ngozi hususan, usoni.

Wapo ambao hujaribu njia mbalimbali za kupunguza makali ya jua, ikiwemo kuvaa miwani, kujifunika na mtandio, kofia au kujifunika mwamvuli.

Pamoja na hayo yote, mtu wa jinsi yoyote, ambaye ana umri wa utu uzima, anashauriwa kutumia mafuta ya kupunguza miale ya jua (sunscreen).

Haya yapo kutoka kampuni mbalimbali na yanapatikana kwa wingi kwenye maduka ya vipodozi.

Mafuta haya yenye muundo wa 'losheni' utayapaka kila siku unapotoka kwenda kwenye mizunguko yako.

Jali ngozi yako kwa kuitunza vyema ili kuepuka magonjwa ya ngozi kama vile saratani.

Afcon 2024



Ni muda, kioo waamuzi kujitazama

Na John MARWA

KATIKA mchezo wa soka kuna sheria 17 zinazotumika kuongoza mchezo huo pendwa na wenye mashabiki kila kona ya Ulimwenguni.

Sheria namba tano na sheria namba sita, zinawazungumzia mwamuzi na waamuzi wasaidizi.

Wakati ambapo Tanzania, Kenya na Uganda ziko mbioni kuhakikisha zinaandika historia ya kuandaa mashindano ya Mataifa ya Afrika; "Pamoja Afcon 2027," eneo muhimu zaidi waandaaji wanaweza kufaidika ni pamoja na kuhakikisha Afrika Mashariki inakuwa na waamuzi wengi zaidi.

ambapo maandalizi yamepamba moto kila nchi ikiwa katika maandalizi ya kufanikisha mashindano hayo makubwa Afrika. Waamuzi wetu wanatambua jembe halimtupi mkulima?

Mwamuzi ndiye anayeongoza mchezo na kutafsiri sheria wakati wa mchezo. Hutoa uamuzi ndani ya kipindi cha mchezo na kutoa taarifa ya mchezo husika baadaye.

Ndiye msemaji au mwamuzi wa mwisho, pale inapobainika kwamba sheria ya mchezo imekiukwa kwa namna yeyote ile, ikiwa ni pamoja na kutoa adhabu pindi mchezaji anapofanya kosa ndani ya uwanja.

Pia kuna waamuzi wasaidizi, hawa ni watendaji wengine wanaomsaidia mwamuzi wa kati wakati mchezo unaendelea. Humsaidia mwamuzi mkuu kuhusu matukio yanayotendeka nje na ndani ya uwanja.

Idadi ya waamuzi wasaidizi hutegemea mashindano au mchezo husika, waamuzi hao hutambulika kama washika vibendera - namba 1&2 na pia kuna kamisaa wa mchezo anayetunza kumbukumbu.

Je, waamuzi wa Afrika Mashariki wanaona fursa yakujisahihisha kupitia Pamoja Afcon 2027?

Ukitazama ukanda wa Afrika Mashariki kumekuwa na uhaba wa waamuzi bora katika mashindano makubwa Afrika, ukiondoa Kenya na Uganda, Tanzania ni nchi isiyoaminika 'kuzalisha' na kuwa na waamuzi wanaoaminika katika michuano mikubwa.

Hata kwenye mashindano ya ndani, kumekuwa na changamoto kubwa na lawama kutokana na makosa wanayoyafanya waamuzi katika michezo ya Ligi Kuu, Championship, Ligi Daraja la Kwanza na Ligi Kuu ya Wanawake.

Acha niwang'ate sikio waamuzi wetu, linalowezekana leo, lisingoje kesho; sasa ni muda wa kujinoa na kuibeba Tanzania na Afrika Mashariki mabegani kwenye Pamoja Afcon.

Huo ni wakati wa kuacha makandokando kwa maslahi mapana ya kazi na hadhi ya mchezo wenyewe.

Nikumbushe kuwa ni aibu kuwa wenyeji wa mashindano na kukosekana watu wenye kupata fursa ya kuwa waamuzi katika Pamoja Afcon 20207.

Kama wenyeji Shirikisho la Vyama vya Soka Afrika Mashariki (Ceacfa) wanapaswa kuwa na mkakati madhubuti wa kuhakikisha nchi waandaaji wanapata idadi ya kuridhisha ya waamuzi katika mashindano hayo makubwa ya Afrika.

Hivi sasa uwe ni mwanzo wa sekta ya waamuzi kuamka na kuwa na weledi, kwani maendeleo ya soka yanawategemea wao.

Waswahili wanasema "kuambiana kupo, kusikilizana hapana." Mimi nimewaambia mkiamua msikilize ama mzibe masikio na kikombe cha aibu tutakinywea sote.



Burudani

Wasanii sita walionufaika na 'bifu'



NEW YORK, MAREKANI

INGAWA bifu, zengwe, mgogoro, kiki, mahusiano ya msanii kwa msanii huchangia kuwasababishia wasanii kutoana uhai, lakini wapo walionufaika.

Baadhi ya wasanii waliopata hasara kwa kutumia njia hizo za bifu ni nguli wa rapu wa Marekani, Amaru Shakur '2Pac' kutoka kundi la Death Law na Notorious 'B.I.G' kutoka kundi la Bad boys.

Ukiondoa hao wapo wasanii sita waliofanikiwa kutokana na kutengeneza bifu akiwemo Kanye West na Taylor Swift, Rihanna na Ciara, Nicki Minaj na Lil Kim

1. KANYE WEST VS TAYLOR SWIFT

Bifu la Taylor Swift na Kanye West lilianzia mwanzoni mwa mwaka 2009 wakati wa utoaji wa tuzo za MTV.

Kanye hakufurahishwa na Taylor Swift kutwaa tuzo ya video bora ya mwaka, kwa kupitia ngoma inayoitwa 'You Belong With Me'.

Kanye alitaka tuzo hiyo ingeenda kwa Queen B kupitia video yake ya 'Single Ladies'.

Baada ya Kanye kusema hayo, Taylor baadaye alimkejeli katika wimbo wake wa 'Look What You made me do'

''Sipendi jukwaa la chini la usemaji ulilojipachika", aliimba.

2. RIHANNA VS CIARA

Bifu jingine lililokolea ni Rihanna 'Riri' na Ciara CiCi' ambao wote walianza muziki mwaka 2005 huku Ciara akipanda katika chati za muziki na wimbo wake Goodies wakati Rihana naye akiwa katika nafasi ya pili na wimbo wake Pon De Replay.

Mashosti hawa wa zamani katika miaka michache iliyopita waliibuka na

upigana vijembe kwenye muziki na baadaye kuhamia kwenye Twitter.

3. NICKI MINAJ VS LIL KIM

Iwapo Rappa yeyote mpya ambaye ni mwanamke ataingia kwenye sanaa ya muziki huo na Lil Kim, asianze naye vita ajue siyo mkali.

Kim ana historia ya kuwavaa wasanii kama vile Eve, Foxy Brown, Remy Ma na wengine wengi akiwemo Nicki Minaj.

Albamu ya Nicki inayokwenda kwa jina la Pink Friday.

Albamu hiyo pamoja na mafanikio lakini Lil Kim aliponda wimbo mmoja uliokuwemo kwnye albamu hiyo wa Black Friday.

Kim alisema Nicki anataka kujifananisha naye. Kauli hiyo ilimuibua Nick Minaj ambaye aliibuka na kumuita 'kahaba mjinga'.



Merino

Klabu ya Arsenal imefikia makubaliano ya kumsajili kiungo Mikel Merino kutoka Klabu ya Real Sociedad kwa ada ya pauni milioni 35. Makubaliano binafsi kati ya mchezaji na klabu yameshafikiwa.

Samardzić



Kiungo wa kati Lazar Samardzić yupo mbioni kujiunga na Klabu ya Atalanta kwa ada ya Euro milioni 20 kutoka Klabu ya Udinese.



Marc Guéhi

Beki wa kati kutoka Klabu ya Crystal Palace, Marc Guéhi yupo mbioni kujiunga na klabu ya Newcastle United, ikumbukwe ofa ya awali ya pauni milioni 60 ilikataliwa na Crystal Palace.

United, Arsenal, Liverpool zaanza vyema EPL

London, England

VIGOGO wa Ligi ya Soka ya England (EPL), wameanza safari ya kusaka ubingwa kwa ushindi mkubwa.

Juzi na jana, timu kubwa za Arsenal, Liverpool na Manchester United, zilianza kwa ushindi, ingawa michezo yao haikuwa rahisi.

Shughuli ilianzia kwenye "matofali ya kuchoma," pale Old Trafford - nyumbani kwa mabingwa wa kihistoria wa EPL Manchester United, ambapo Agosti 16, miamba hiyo ikianza kwa kubeba pointi tatu muhimu baada ya kuifunga Fulham kwa bao 1-0. Kupitia kwa kijana Joshua Zirkzee "dakika za jioni."

Mitanange mingine iliendelea Juzi - Jumamosi ambapo viwanja sita viliwaka moto. Majogoo wa Liverpool waliwafuata Ipswich na kuwakanda mabao 0-2 kupitia kwa Diogo Jota na Mohamed Salah.

Kazi iliendelea katika viwanja vingine ambapo Nottingham walitoka suluhu dhidi ya Bournemouth, katika dimba la St. James' Park Newcastle wakaibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Southampton.

Everton wakiwa nyumbani kwao, Goodison Park walikutana na miguu ya bajaji (0-3) kutoka kwa Brighton; Arsenal 'The Gunners' wakawashinda nyumbani kwa mabao 2-0 mbele ya Wolves; "wagonga nyundo" wa London - Newcastle wakalala nyumbani kwa kichapo cha mabao (1-2) kutoka kwa Aston Villa.

Jana – Jumapili, Brentford waliwanyuka Crystal Palace mabao (2-1), huku Chelsea na Manchester City wakionyesha ubabe.

Moja ya matukio yaliyoingia kwenye vitabu vya EPL msimu huu ni bao la kwanza la msimu kutoka kwa kijana wa Manchester United, Joshua Zirkzee, huku Fabian Schar nyota wa Newcastle United, akiwa mchezaji wa kwanza kuonyeshwa kadi nyekundu dakika ya 28 ya mchezo dhidi ya Southmpton, akiungana na Ashley Young wa Everton naye aliyekula umeme dakika ya 66 ya mchezo dhidi ya Brighton.

Timu ambazo hazijafunga bao katika mchezo wao wa kwanza msimu huu ni Fulham, Ipswich, Southmpton, Everton na Wolves, huku ni mchezo mmoja tu ulimalizika kwa sare ya bao (1-1) Nottingham dhidi ya Bournemouth.

Leo, Jumatatu kutakuwa na mchezo mmoja 'Monday Football Night' Leicester City wakiwaalika Tottenham Hotspurs kukamilisha mzunguko wa kwanza.



Kiungo wa Arsenal, Bukayo Saka.

MICHEZO
Jumatatu, Agosti 19 - 25, 2024



Makali ya Fadlu yameanza mapema



Kiungo wa Simba, Kibu Denis (kushoto), akiwa na Awesu Awesu, wakati wakishangilia bao la tatu lililolifungwa na Awesu jana kwenye mchezo dhidi ya Tabora United ambapo Simba walishinda 3-0. (Picha na SC)

Na John MARWA

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Simba, Fadlu Davis "sasa ameanza kazi" baada ya kikosi chake kuirarua Tabora United kwa mabao 3 - 0.

Mtanange huo ulipigwa jana katika Dimba la KMC, Mwenge, Dar es Salaam.

Ulikuwa mchezo wa kwanza kwa Simba kutupa karata zake msimu huu wa Ligi Kuu ya Soka Tanzania Bara (NBC PL) 2024/2025 wakiwa na kikosi kipya na benchi jipya la ufundi.

Simba waliingia kwenye mchezo huo wakihitaji pointi tatu muhimu ili kuanza kuusaka ubingwa wa ligi walioupoteza kwa misimu mitatu mtawalia mbele ya watani wao wa jadi, Yanga SC.

Haukuwa mchezo rahisi hasa kipindi cha kwanza ambapo wapinzani wao klabu ya Tabora United walikaa nyuma muda mwingi kuwanyima Simba nafasi ya kufanya wanachotaka, hasa kwenye eneo lao la ulinzi.

Licha ya kupaki basi, bado Simba alifanya mawindo yake taratibu na kufanikiwa kupata mabao 3 kupitia kwa nyota wake; Chemalone Fondo dakika ya 14, Valentino Mashaka na Awesu Awesu awaliofunga kipindi cha pili na kuipatia Simba pointi tatu na mabao matatu.

Kwa ushindi huo, Simba wamekaa kileleni mwa ligi licha ya kuwa wapinzani wao wa karibu Yanga na Azam FC wao hawakucheza kutokana na kuwa na majukumu ya michezo ya awali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika michuano hiyo ya kimataifa, Yanga walianza kampeni yao kwa kushinda ugenini kwa mabao 0-4 dhidi ya Vital'o ya Burundi, huku mchezo wa marejeano ukiwa ni Jumamosi ya wiki hii katika Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION